# UFASIRI KIPRAGMATIKI WA DISKOSI KATIKA GAZETI LA *TAIFA LEO* JUU YA UHIFADHI WA MISITU KENYA

NA

CHARLES OMUKUBA MUSAMALI

TASNIFU ILIYOWASILISHWA KAMA SEHEMU YA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA

CHUO KIKUU CHA MASENO

© 2013

MASENO UNIVERSITY
S.G. S. LIBRARY

# IKISIRI

Matumizi ya mikakati mbalimbali ya kipragmatiki katika diskosi huweza kuzua utata katika kufasiri ujumbe ulionuiwa kumfikia msomaji au msikilizaji. Tamko la msemaji au mwandishi fulani huweza kufasiriwa na msikilizaji au msomaji kwa njia mbalimbali. Hali kama hii huibua maana mbalimbali za ujumbe mmoja ambapo mawasiliano hutatizika. Utafiti huu ulinuia kubaini jinsi mikakati ya kipragmatiki inavyodhihirika katika diskosi za uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya. Vile vile utafiti huu ulinuia kuonyesha jinsi mikakati hiyo inavyoathiri ufasiri wa ujumbe unaodhamiriwa na mwandishi hivyo basi kutatiza juhudi za serikali za kuhifadhi misitu. Malengo ya utafiti huu yalikuwa: Kubaini mikakati ya kipragmatiki inayotumiwa katika diskosi za uhifadhi wa misitu ili kupitisha ujumbe ulionuiwa na mwandishi, kujadili njia mbalimbali zinazotumiwa na umma kufasiri maana katika habari juu ya uhifadhi wa misitu na mwisho, kueleza athari ya ufasiri wa kipragmatiki wa habari juu ya uhifadhi wa misitu kwa shughuli za uhifadhi wa misitu. Nadharia ya kipragmatiki ya 'umaanishi wa kimaongezi' ya Grice ilituongoza katika utafiti huu. Data kuhusu mikakati mbalimbali ya kipragmatiki katika diskosi ya uhifadhi wa misitu ilikusanywa kwa njia ya uchanganuzi wa yaliyomo ambapo nakala zote 36 za magazeti ya *Taifa Leo* ya mwaka baina ya 2008 na 2009 zilihusishwa. Mikakati mbalimbali ya kipragmatiki kama vile, matumizi ya jazanda, kinaya, umaanisho, semi, vionyeshi na matumizi ya uongo ilibainishwa. Hojaji iliyotayarishwa na mtafiti kwa kuzingatia mada ya utafiti huu ilitumiwa kukusanya data kutoka kwa umma. Jumla ya watu wazima 50 wenye umri wa miaka 18 na zaidi na wanaojua kusoma na kuandika kutoka katika eneo la Msitu wa Kakamega haswa kata za Lukusi, Ivihiga, Kambiri na Lubao waliokuwa wakihudhuria mabaraza ya chifu walijitokeza kuhojiwa. Wahojiwa hao walipokezwa hojaji ambapo walizijaza kwa kuzingatia maswali yaliyokuwa yameulizwa. Aidha utafiti huu ulidhihirisha kuwa matumizi ya kinaya na jazanda katika habari juu ya uhifadhi wa misitu ndiyo husababisha ufasiri uliopotoka wa kiwango cha juu zaidi-asilimia 64% na 42% mtawalia. Utafiti huu vilevile ulidhihirisha kuwa ufasiri wa kipragmatiki wa habari juu ya uhifadhi wa misitu na umma una athari hasi katika shughuli za uhifadhi wa misitu. Kutokana na matokeo ya utafiti huu mapendekezo yafuatayo yalitolewa: Uhariri wa habari zinazochapishwa katika gazeti la *Taifa Leo* juu ya uhifadhi wa misitu ufanywe kwa misingi ya kuhakikisha kuwa utata wa ufasiri wa habari unaotokana na kuwepo kwa mikakati ya kipragmatiki umepunguzwa kabisa kama sio kuondolewa.

# ABSTRACT

The use of pragmatic strategies in a given discourse is likely to cause a challenge in interpretation of information communicated by a speaker or a writer. An utterance by a speaker is likely to be interpreted by the listener in various ways thus giving varied meanings. Such a situation whereby various meanings are derived from a given discourse may lead to communication breakdown. This research intended to establish the existence of pragmatic strategies and find out how such strategies in discourse on forest conservation affect the interpretation of information on forest conservation intended by the writer therefore rendering the efforts on forest conservation by the government futile. The basic objectives for this research were: to establish the pragmatic strategies used in the discourse on forest conservation, to discuss the various strategies used by the audience to interpret the information on forest conservation and lastly, to explain the effects of pragmatic interpretation of the information on forest conservation activities. The Gricean Theory of Conversational Implicature was applied in this research. Data on the various pragmatic strategies used in discourse on forest conservation was collected through content analysis method whereby all the 36 copies of *Taifa Leo* newspaper of the year 2008 and 2009 that contained information on forest conservation were used. Various pragmatic strategies such as metaphor, irony, implicature, sayings, demonstratives and the use of lies in the discourse on forest conservation in the 36 copies of the *Taifa Leo* newspaper were identified. A self-formulated questionnaire based on the topic of research was used to collect information on public interpretation of information on forest conservation. A total of 50 literate adult citizens aged 18 years and above residing around Kakamega forest specifically in Lukusi, Ivihiga, Kambiri and Lubao locations volunteered to respond to the questionnaire. The research established that the use of pragmatic strategies such as metaphor and irony led by 64% and 42% respectively in below average interpretation of information on forest conservation. The research also found out that a pragmatic interpretation of information on forest conservation by the public had a negative effect on the forest conservation activities. Based on the findings of this research the following recommendation was made: The editing of the information on forest conservation that is usually published in the *Taifa Leo* newspaper, should be thoroughly done, with a view of completely reducing if not removing, any misinterpretation by the public because of the use of pragmatic strategies in such information.



MASENO UNIVERSITY
S.G. S. LIBRARY

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

Katika utafiti huu, uchanganuzi wa ufasiri kipragmatiki wa diskosi andishi ya uhifadhi wa misitu nchini Kenya ulifanywa. Diskosi za uhifadhi wa misitu zilichanganuliwa kwa lengo la kubainisha mikakati mbalimbali ya kipragmatiki ambayo huenda hutatiza umma katika kufasiri habari za uhifadhi wa misitu nchini Kenya. Utafiti mzima umegawanywa katika sura tano ambazo ni; utangulizi, mapitio ya maandishi, njia na mbinu za kukusanya data, uchanganuzi wa data na mwisho, hitimisho. Baadhi ya vipengele vilivyowasilishwa katika sura hii ya kwanza ni pamoja na; usuli wa utafiti ambapo dhana zinazopatikana katika mada ya utafiti huu zimeelezwa kwa kuwarejelea wataalamu mbalimbali. Suala la utafiti huu limeelezwa. Maswali ya utafiti pamoja na malengo ya utafiti huu yametajwa kwa kuorodheshwa bayana. Upeo wa utafiti huu vilevile umeelezwa ambapo sampuli iliyotumika katika utafiti huu imeelezwa. Mbali na sampuli iliyotumika katika utafiti huu, eneo ambako utafiti huu ulifanyiwa-Msitu wa Kakamega limefafanuliwa. Katika sura hii, misingi ya uteuzi wa mada ya utafiti huu pamoja na umuhimu wake umezungumziwa na mtafiti. Hatimaye, nadharia iliyotumika katika kufanya utafiti huu – nadharia ya uamali ya umaanishi wa kimaongezi ya Grice (1975) imefafanuliwa waziwazi ili kuonyesha jinsi nadharia hiyo ilivyomsaidia mtafiti kuafikia madhumuni ya utafiti huu.

### 1.1 Usuli wa Utafiti

Lugha ni chombo muhimu na cha kimsingi katika mawasiliano. Kwa misingi hii, ni muhimu kuelewa jinsi lugha hutumiwa katika mawasiliano ili kufanikisha juhudi za kupitisha ujumbe kutoka kwa msemaji au mwandishi hadi kwa hadhira yake. Kukosekana kwa ufahamu wa aina hii huenda ukasababisha kukatika kwa mawasiliano baina ya wanaohusika.

Dasgupta (1993), anatambua kuwa mawasiliano-shirikishi ni kiwango cha juu cha kuwashirikisha raia katika kufikia matamanio yao. Kiini ni kwamba dhana ya mawasiliano hurejelea kanuni za kisaikolojia, kitamaduni na kijamii na hivyo ufahamu na uwezo wa kutumia lugha katika kueneza habari huakisi umilisi wa kimawasiliano miongoni mwa



MASENO UNIVERSITY
S.G.S. LIBRARY

wanaohusika. Kwa misingi hiyo, utafiti huu ulilenga kuchunguza iwapo habari zinazotolewa juu ya uhifadhi wa misitu zinaakisi hali za wanaolengwa kisaikolojia, kitamaduni na kijamii ili kufanikiwa katika kuwashirikisha katika uhifadhi wa misitu nchini Kenya. Mikakati mbalimbali ya kipragmatiki ilibainishwa katika diskosi ya uhifadhi misitu na kuonyesha jinsi inavyoathiri wasomaji katika kufasiri ujumbe ulionuiwa na mwandishi.

Kwa upande mwingine, Hofmann (1993), anasema kuwa mawasiliano ni ushirikiano kati ya mzungumzaji na anayezungumziwa. Anaendelea kusema kuwa ni lazima maneno yateuliwe vilivyo ili kusudi la mawasiliano lieleweke na pia anayezungumziwa aweze kufasiri yaliyokusudiwa na mzungumzaji kwa kurejelea muktadha wa mazungumzo. Kwa mujibu wa Malinowski (2012), umilisi wa kipragmatiki ni uwezo wa kufahamu au kuelewa maana kipragmatiki iliyonuiwa na msemaji wa tamko. Malinowski (2012), anaendelea kusema kuwa uelewo wa kipragmatiki huchukuliwa kuwa sehemu iliyo na changamoto kubwa sana katika kujifunza lugha. Licha ya kuwa hali hii huweza kufunzwa, aghalabu tajiriba ya anayefunzwa ndiyo njia ya pekee ya kuweza kupata umilisi huo wa kipragmatiki. Ili kuweza kufasiri maana ya tamko la sentensi yoyote ile, kinachohitajika kuzingatiwa kwanza ni muktadha wa tamko hilo kisha mazingira yake. Mambo hayo mawili yatatuwezesha kupata maana ya tamko la sentensi husika. Maelezo hayo yanatuelekeza kwa maana ya ufasiri kipragmatiki ambayo ni ufafanuzi wa maana ya tamko la msemaji kwa misingi ya kipragmatiki huku muktadha na mazingira ya tamko husika yakitiliwa maanani. Katika utafiti huu, fasiri za umma juu ya diskosi za uhifadhi wa misitu zitachanganuliwa ili kuona iwapo umma unafasiri vilivyo diskosi hizo kwa misingi ya kipragmatiki.

Sperber & Wilson (1995), wanaongezea kuwa muktadha unaweza kuchukuliwa kama sehemu tu ya yanayodhaniwa kuhusu dunia na anayepokea habari. Ni huku kudhania ndiko kunakoathiri ufasiri wa matamshi. Hali kama hii huweza kuwa na matokeo mabaya zaidi katika kujaribu kufasiri lugha. Ni kutokana na misingi hii ndipo utafiti huu ulifanya uchunguzi wa iwapo kufasiriwa kwa habari za kuhimiza uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo* na umma kunaweza kuwa na utata wowote na hivyo basi kufanya juhudi za kuhifadhi misitu kutofaulu.

Aidha, Bloomer, Griffiths & Merrison (2005), wanaeleza pragmatiki kuwa taaluma inayochanganua lugha kimuktadha. Taaluma hii huangazia jinsi wazungumzaji wa lugha

wanavyotumia ufahamu wao kuwasilisha maana. Pragmatiki huchunguza jinsi lugha hutumiwa katika kufasiri matamshi na maana. Utafiti huu ulidhamiria kuchanganua diskosi zilizoandikwa katika gazeti la *Taifa Leo* juu ya uhifadhi wa misitu nchini Kenya ili kubaini jinsi maana zilizokusudiwa zinavyofasiriwa kwa misingi ya kipragmatiki na hadhira na kueleza jinsi ambavyo fasiri za aina hiyo huathiri juhudi za uhifadhi wa misitu.

Kwa mujibu wa Van Dijk (1981), diskosi ni tamko la lugha ya kawaida iliyo na mfuatano wa sentensi unaoafikia utaratibu wa kiisimu kama vile sintaksia, semantiki na hata pragmatiki. Ni sharti mshikamano katika diskosi udhihirike ili tamko hilo liweze kukubalika kuwa diskosi. Kwa upande wake, Mills (1997) anaeleza diskosi kuwa maendelezo na matumizi ya maongezi au maandishi ambapo huwa na urefu wa zaidi ya sentensi moja. Anazidi kufafanua uchanganuzi wa diskosi kuwa hali ya kusoma kwa makini na kutathmini mshikamano na mahusiano mengine kati ya sentensi katika diskosi andishi au matamshi. Katika utafiti huu, tulijikita katika uchanganuzi wa diskosi andishi ya uhifadhi wa misitu nchini Kenya ambapo mikakati mbalimbali ya kipragmatiki kama vile umaanisho, kinaya, jazanda na hata matumizi ya semi miongoni mwa mikakati mingine ilibainishwa na kuchanganuliwa ili kuonyesha jinsi mikakati hiyo huathiri ufasiri wa habari katika diskosi hizo za uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo*.

Otiende, Ezaza & Boisvert (1991), wanaeleza mazingira kama neno linalotumiwa kuelezea yale yote yanayomzingira mwanadamu pamoja na rasilimali zote anazoweza kuzifikia katika eneo lake na kuzitumia kwa manufaa yake. Misitu ni mojawapo ya rasilimali muhimu zilizoko katika mazingira ya binadamu na ambazo amezitumia ili kujinufaisha kwa namna mbalimbali. Kwa mujibu wa Cotthem (2009), msitu ni eneo la zaidi ya ekari moja lililo na miti ambayo ina urefu wa zaidi ya mita tano. Miti hii ni sharti iwe imefunika eneo hilo kwa asilimia arobaini (40%). Brenton (1994), akielezea umuhimu wa misitu, anasema kuwa misitu huvutia mvua, huwa vianzo vya mito mbalimbali, hushikilia udongo na kuwa maskani ya wanyama pori. Licha ya umuhimu huu wa misitu, rasilimali hii muhimu imekabiliwa na hatari kubwa ya kuangamia kutokana na watu kutozingatia habari zinazotolewa kuhusu uhifadhi wa misitu (Gichiri, 2009). Katika utafiti huu, tulichukulia dhana ya msitu kumaanisha eneo lolote lile lililopandwa miti.

Allison (2009), anaelezea uhifadhi wa misitu kama hali ya kutunza na kuirudisha misitu katika hali nzuri, kuilinda dhidi ya uharibifu na kutoijali. Uhifadhi wa misitu ulichukuliwa na utafiti huu kuwa hali ya kuitunza misitu kwa kutoikata miti kiholela au kuiharibu miti inayopatikana katika msitu husika. Vile vile watu wanaoishi katika maeneo ya misitu walitarajiwa kufasiri habari kuhusu uhifadhi wa misitu kwa namna inayodhihirisha juhudi zao za kuwa tayari kuhifadhi miti ili kuziba pengo lililoachwa baada ya kuiharibu miti kwa matumizi yao yaliyo na umuhimu.

Wananchi wa Kenya walioivamia misitu na kujenga makao huko walitarajiwa wawe tayari kuhama kutoka misituni ili kuipa misitu hiyo fursa ya kunawiri. Aidha ilitarajiwa kuwa shughuli mbalimbali kama vile upanzi wa vyakula na kulisha mifugo katika maeneo ya misitu zingekomeshwa ili misitu iweze kustawi. Ukubalifu wa ushauri kutoka katika wizara ya misitu, wanasiasa na mashirika mbalimbali yanayohusika na uhifadhi wa misitu ungechukuliwa kuwa ishara nzuri ya kuonyesha nia ya walioivamia misitu hiyo kuhifadhi misitu. Utafiti huu ulichunguza iwapo ufasiri wa habari juu ya uhifadhi wa misitu visivyo ulitokana na kutozingatia mikakati ya kipragmatiki na ambayo huenda ndiyo sababu ya kutofaulu kwa juhudi za kuhifadhi misitu nchini Kenya. Uhifadhi wa misitu ni suala ambalo limehimizwa kupitia njia mbalimbali za mawasiliano kwa watu na nchi nyingi duniani haswa nchi ya Kenya. Himizo hili limetokana na umuhimu mkubwa ambao binadamu ameipa misitu. Misitu humfaidi binadamu kwa njia mbalimbali kama vile kuwa hifadhi ya wanyama wa porini, kuzalisha malighafi ya viwanda, kuwa chemichemi ya mito na hata kuwa kivutio cha mvua miongoni mwa faida nyinginezo. Licha ya umuhimu huo, juhudi za kuhifadhi misitu bado zinakumbwa na changamoto nyingi. Misitu imeharibiwa kwa kukatwa kiholela na watu ambao aidha wanapanua makazi yao au wanatafuta tu rasilmali ipatikanayo misituni humo. Mfano mzuri ni ule wa msitu wa Mau ambapo watu wanaokaa msituni humo walikataa wito wa serikali wa kuwataka waondoke msituni humo ili msitu uweze kuhifadhiwa. Ilibidi serikali kuwatimua watu hao kutoka msitu huo kwa lazima suala ambalo lilizua tetesi kali kutoka kwa makundi mbalimbali kama vile watetezi wa haki za binadamu, wanasiasa na kadhalika.

## 1.2 Suala la Utafiti

Pragmatiki ni taaluma inayojihusisha na uchunguzi wa lugha kimuktadha. Taaluma hii huchunguza na kueleza jinsi matamshi au maandishi hufasiriwa na wasikilizaji au wasomaji wa diskosi husika. Fasiri za habari inayowasilishwa na mwandishi au msemaji fulani huweza kuzua utata kwani anayepokea habari husika huweza kuchukulia muktadha uliolengwa kama sehemu tu ya yale yanayodhamiriwa na msemaji au mwandishi. Hali kama hii hutokea kwa sababu tamko moja la mzungumzaji au mwandishi huweza kufasiriwa kwa njia tofauti tofauti. Baadhi ya fasiri hizo huwa potovu, hali ambayo hukatiza mawasiliano. Mikakati mbalimbali ya kipragmatiki ambayo hutumika na mwandishi au mzungumzaji wa habari husika huchangia pakubwa katika kutatizika kwa kueleweka kwa habari iliyowasilishwa kwa hadhira. Lugha kama kipengele cha kimsingi cha mawasiliano ni muhimu katika kufanikisha juhudi za kuhifadhi misitu iwapo itatumiwa kwa ufahamu kuwa ina uwezo mkubwa wa kuchangia katika kutatua baadhi ya matatizo yanayoikumba jamii. Ni kutokana na hali hii ndipo utafiti huu ulikusudia kuchanganua kwa njia ya kipragmatiki, diskosi zinazochapishwa katika gazeti la *Taifa Leo* kuhusu uhifadhi wa misitu ili kubaini namna maana mbalimbali zinazoweza kufasiriwa katika diskosi hizo, zinavyoathiri umma katika juhudi za kuhifadhi misitu. Utafiti huu ulikusudia kuchunguza iwapo upuuzaji wa mikakati ya kipragmatiki katika kufasiri maana zipatikanazo katika diskosi za uhifadhi wa misitu huchangia katika ufasiri uliopotovu hali ambayo huenda ndiyo hupelekea kutofaulu kwa juhudi za kuhifadhi misitu.



MASENO UNIVERSITY
S.G. S. LIBRARY

## 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu ulitarajia kujibu maswali yafuatayo:

1. Je, ni mikakati gani ya kipragmatiki inayotumiwa katika diskosi juu ya uhifadhi wa misitu ili kuwasilisha ujumbe na maana zilizokusudiwa?
2. Umma unatumia njia zipi ili kufasiri maana katika habari juu ya uhifadhi wa misitu?
3. Ni athari zipi zinazotokana na ufasiri wa kipragmatiki wa habari juu ya uhifadhi wa misitu kwa shughuli za kuhifadhi misitu?

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuchanganua ufasiri kipragmatiki wa habari kuhusu uhifadhi wa misitu nchini Kenya. Utafiti huu ulijikita katika malengo mahsusi yafuatayo:

1. Kubaini mikakati ya kipragmatiki inayotumiwa katika diskosi juu ya uhifadhi wa misitu ili kupitisha ujumbe ulionuiwa.
2. Kujadili njia mbalimbali zinazotumiwa na umma kufasiri maana katika habari juu ya uhifadhi wa misitu.
3. Kueleza athari zinazotokana na ufasiri wa kipragmatiki wa habari juu ya uhifadhi wa misitu kwa shughuli za kuhifadhi misitu.

## 1.5 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu unahusu uchanganuzi wa ufasiri kipragmatiki wa diskosi ya uhifadhi wa misitu nchini Kenya. Uchanganuzi ulifanyiwa habari zilizoandikwa katika gazeti la *Taifa Leo* na ambazo zilihusu uhifadhi wa misitu nchini Kenya. Habari zilizochapishwa katika gazeti la *Taifa Leo* kuhusu shughuli za uhifadhi wa misitu zilichanganuliwa. Jumla ya nakala 36 za matoleo ya gazeti la *Taifa Leo* za mwaka baina ya 2008 na 2009 zilitumiwa katika uchanganuzi huo kwa kutumia muundo mseto wa kinathari na kitakwimu. Jumla ya

wahojiwa hamsini (50) kutoka eneo la Msitu wa Kakamega walijitokeza kujaza hojaji ambayo walipokezwa na mtafiti.

### 1.6 Misingi ya Uteuzi na Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ulihusu ufasiri kipragmatiki wa habari zilizochapishwa kwenye gazeti la *Taifa Leo* na ambazo zinahusu uhifadhi wa misitu nchini Kenya. Wataalamu kama vile Gichiri (2009) wanasema kuwa eneo lililofunikwa na misitu nchini Kenya ni asilimia ishirini (20%) kiwango ambacho ni cha chini sana kikilinganishwa na kile kilichowekwa na Umoja wa Mataifa cha asilimia arobaini (40%). Gichiri (2009) anaendelea kusema ya kwamba kuna haja ya dharura ya kueneza habari kuhusu uhifadhi wa misitu nchini Kenya hususan Msitu wa Mau. Brenton (1994) katika utafiti wake, anatambua kuwa licha ya habari juu ya uhifadhi wa misitu kuenezwa kote duniani, bado uharibifu wa misitu katika eneo la nchi zilizo na joto jingi kote duniani, Kenya ikiwa mojawapo wa nchi hizo, ni wa kiwango cha juu sana-asilimia moja (1%). Uharibifu huu umezidi kuongezeka katika siku za hivi karibuni licha ya hali ya mawasiliano kuimarika. Kwa mfano, miaka ya hivi karibuni imeshuhudia mhemko mkubwa kuhusu haja ya kuhifadhi misitu nchini Kenya hususan msitu wa Mau, Kakamega, Mlima Kenya, Mlima Elgon, Aberdares na vilima vya Cherengani. Uharibifu wa misitu hiyo ilipelekea kukauka kwa mito mingi nchini Kenya. Vilevile, nchi ilishuhudia kipindi kirefu cha ukame. Hali hii ilikuwa na madhara makubwa sana kwa jamii mbalimbali nchini Kenya na eneo zima la Afrika Mashariki kwa ujumla.

Kwa mujibu wa UNEP (1999), sababu za kijumla kuhusu kuzorota kwa hali ya mazingira sio ukosefu wa ufahamu kuhusu madhara ya kimazingira yanayoukumba ulimwengu mzima bali ni ukosefu wa mawasiliano kati ya makundi mbalimbali yanayodhamini utatuzi wa matatizo hayo na wanaoathiriwa na matatizo hayo. Kwa hivyo, mada hii ilichaguliwa ili kuchangia katika kutatua matatizo ya kimawasiliano, yaani upuuzaji wa mikakati ya kipragmatiki, ambayo huenda yanachangia katika kudorora kwa juhudi za kuhifadhi misitu nchini Kenya.

Ni muhimu kutambua jinsi maana mbalimbali zinavyofasiriwa kwa misingi ya kipragmatiki katika diskosi andishi juu ya uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo*. Hali kama hii huenda huchangia katika kutofaulu kwa juhudi za serikali za uhifadhi wa misitu nchini

Kenya. Maana tofauti tofauti zinazofasiriwa na wanaosoma habari katika gazeti la *Taifa Leo* huweza kusababisha utata katika kuelewa kile kilichonuiwa na wanaotoa habari hizo. Ni bora kurekebisha hali kama hii ili ujumbe unapotolewa kuhusu uhifadhi wa misitu, hadhira husika ipate maana bwiwa moja kwa moja bila kukanganyika.

Data ambayo iliibuliwa na utafiti huu ilitarajiwa kuwa ingetumiwa kutoa mapendekezo ambayo yangekuwa muhimu katika kufanikisha juhudi za kuhifadhi misitu nchini Kenya. Wahariri wa gazeti la *Taifa Leo* wataweza kutumia data hiyo ili kuboresha uhariri wao kwa minajili ya kuondoa utata unaoweza kuzuka wakati wasomaji wa gazeti la *Taifa Leo* (umma) wanapozisoma habari nyinginezo na haswa zile zinazohusu uhifadhi wa misitu na hivyo basi kuepuka kupotosha ujumbe ulionuiwa kumfikia msomaji kuhusu uhifadhi wa misitu nchini Kenya.

Aidha taaluma ya isimu haitakosa kufaidika na matokeo ya utafiti huu kwani maelezo ya mikakati ya kipragmatiki katika habari za lugha ya Kiswahili kama yalivyojitokeza katika diskosi za uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo* yametoa mchango si haba.

Waunda sera za uhifadhi wa misitu wataweza kutambua umuhimu wa kuandika habari isiyokuwa na utata mwingi ili wasomaji wake waweze kuupata ujumbe ulionuiwa kumfikia msomaji ili aweze kushiriki katika juhudi za kuhifadhi misitu kikamilifu.

Hatimaye, utafiti huu unaweza kuwa msingi mzuri kwa utafiti mpana kuhusu mada hii au mada na nyanja nyingine kama vile za matibabu, elimu na kadhalika ambapo watafiti wataonyesha jinsi fasiri mbalimbali za ujumbe kwa misingi ya pragmatiki zinavyoweza kutatiza mawasiliano katika nyanja hizo.

## 1.7 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uamali ya 'umaanishi wa kimaongezi' ya Grice. Nadharia hii iliasisiwa naye Grice (1975) na mawazo hayo kuendelezwa na Leech (1983), Grundy (2000) na Bloomer & et al (2005) miongoni mwa wengine. Kwa mujibu wa nadharia hii mawasiliano ni ushirika kati ya mzungumzaji na hadhira yake. Ni lazima anayezungumza ateue maneno yake vilivyo ili msikilizaji aweze kuelewa dhamira ya mawasiliano na vile vile

aweze kung'amua alichomaanisha mzungumzaji. Grice (1975) alijitokeza na nadharia hii katika juhudi za kujaribu kueleza na kutabiri umaanishi utokanao na mazungumzo kati ya wahusika wawili. Ili kueleza dhana aliyokuwa nayo, Grice (1975) alirejelea kategoria zifuatazo:

1. Kategoria ya kiasi. Kategoria hii inahusu kiasi cha ujumbe ambao wahitajika. Mzungumzaji au mwandishi sharti ayafanye maandishi au mazungumzo yake yamfahamishe msikilizaji au msomaji kadri iwezekanavyo. Vile vile, mwandishi au mzungumzaji asizidishe habari katika maandishi au mazungumzo yake kupita kiasi.
2. Kategoria ya ubora inamhimiza mwandishi au mzungumzaji kutosema kile ambacho anaamini kuwa ni uwongo. Vile vile mzungumzaji au mwandishi hapaswi kusema au kuandika kile asichoweza kudhibitisha.
3. Kategoria ya kufungamana na mada. Ni sharti mzungumzaji au mwandishi azungumze au aseme mambo ambayo yanafungamana na mada husika.
4. Kategoria ya jinsi. Mzungumzaji au mwandishi anahitajika kutofumba mazungumzo au maandishi yake, kutozua utata katika mazungumzo au maandishi yake, mazungumzo au maandishi yasiwe marefu kupindukia bali yawe ya kiasi cha kutosha kupitisha ujumbe tu na mazungumzo au maandishi yafuate utaratibu maalumu unaoeleweka bila kutatiza anayeupokea ujumbe husika.

Mbali na kanuni hizo nne, Grice (1975) alirejelea dhana ya ushirika ambapo anasema ya kuwa kanuni hii inahimiza washiriki katika mazungumzo kuchangia mazungumzo inavyohitajika katika kiwango kinachofaa kulingana na mielekeo mwafaka ya mazungumzo.

Habari kuhusu uhifadhi wa misitu inapoandikwa bila kuteua maneno ipaswavyo ili dhamira ya ujumbe huo itambulike, hadhira huenda ikakanganyika na hivyo basi kukosa kutimiza kilichonuiwa na msemaji au mwandishi wa habari zinazohusika – kuhifadhi misitu.

Grundy (2000) anasema kuwa ili kutatua tatizo la jinsi tunavyomwelewa mzungumzaji kumaanisha mambo ambayo kwa hakika hasemi, ni lazima kwanza tuweke mpaka kati ya maana asilia na maana isiyo asilia ya usemi wa mzungumzaji. Kwa mfano, tunaposema:

*Timu yetu ya kandanda ilishinda.* (Tafsiri yangu)

Jambo linaloeleweka hapa ni kwamba hiyo timu ilifunga angalau bao moja zaidi ya timu pinzani kwani hakuna jinsi ambavyo timu ya kandanda inaweza kushinda bila kuongoza kwa ufungaji mabao. Hii ni maana bwiwa ambayo huwa inapatikana katika tamko lolote lile la mzungumzaji. Hata hivyo maana isiyo asilia katika sentensi hiyo ni kuwa timu husika ilishinda kwa kucheza mchezo murua na hivyo kuilemea timu pinzani. Kwa hivyo mpaka utakaochorwa kati ya maana hizo mbili utamwezesha msikilizaji kuelewa maana aliyonuia mzungumzaji wa usemi wowote ule. Grundy (2000) anaendelea kusema ya kuwa wazungumzaji huwa wamenuia kuwa na ushirikiano wanapozungumza. Ushirika huo unafaa kudhihirika kwa mzungumzaji kutoa habari ya kutosha ili kuondoa utata wowote ambao huenda ukasababisha ujumbe kutopatikana na msikilizaji. Utafiti huu ulilenga kubaini iwapo habari zinazotolewa katika gazeti la *Taifa Leo* kuhusu uhifadhi wa misitu nchini Kenya zinadhihirisha kukosekana kwa ushirikiano kati ya anayetoa habari kuhusu uhifadhi wa misitu na yule aliyelengwa na hivyo basi kumfanya aliyelengwa kukosa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi misitu.

Kwa mujibu wa Bloomer & et al (2005), kategoria nne za mazungumzo zilizowekwa naye Grice zinasaidia katika kuhakikisha ya kuwa ujumbe ulionuiwa na mzungumzaji kuifikia hadhira yake haupotoshwi kamwe. Akielekea kukubaliana naye Bloomer & et al (2005), Indede (2007), anairejelea kanuni ya ushirika, (*Cooperative Principle*) yake Grice (1975) kama msingi wa mawasiliano. Katika kufaulisha mawasiliano, kategoria nne zilizotolewa naye Grice (1975) ni muhimu sana kuzingatiwa. Wataalamu hao wawili wanatambua umuhimu wa nadharia ya Grice (1975) ya umaanishi wa kimaongezi katika kuelewa na kufasiri vilivyo habari inayopitishwa na mzungumzaji. Utafiti huu ulitumia nadharia hiyo ili kueleza jinsi umma unavyofasiri habari juu ya uhifadhi wa misitu nchini Kenya katika gazeti la *Taifa Leo*.

Kwa upande wake, Leech (1983) anaongezea kauli nyingine muhimu kama vile, kauli ya upole na kejeli ambazo zikizingatiwa hufanikisha mawasiliano kati ya msemaji na hadhira yake. Anaporejelea nadharia ya Grice ya umaanishi wa kimaongezi, Leech (1983), anatambua kuwa kauli za ushirikiano na upole katika maongezi ni muhimu sana katika kufaulisha mawasiliano. Hata hivyo kauli ya ushirikiano pekee haiwezi kusaidia kuelezea ni kwa nini, kwa mfano, watu huwa hawawasilishi ujumbe wao moja kwa moja ili maana

iliyodhamiriwa ijitokeze wazi wazi. Hali kama hii huweza kuelezewa tu kwa kurejelea kauli ya upole. Leech (1993) anarejelea majadiliano kati ya wahusika wawili, *A* na *B* wanapojadiliana juu ya wenzao ambao wamepata uhamisho. Tunaona jinsi ambavyo mhusika *B* anavyoamua kuzingatia kauli ya upole katika jawabu lake. Tazama majadiliano yao:

*A*: *Tutawakosa Bill na Agatha ama sivyo*?

*B*: *Naam, sote tutamkosa Bill*. (Tafsiri yangu)

Katika muktadha huu, mhusika *B* anakosa kuzingatia kauli ya kiasi anapokosa kutoa habari ya kina kuhusiana na swali aliloulizwa na mwenzake *A*. Katika hali hii, tunaweza kukisia umaanisho wake *B* kwamba hatamkosa Agatha na anafanya hivyo kwa kuzingatia kauli ya upole badala ya kauli ya kiasi ili asimuudhi mhusika wa tatu ambaye ni Agatha.

Kwa kulinganisha kauli hizi mbili-kauli ya ushirikiano na kauli ya upole, Leech (1983) anahoji kuwa kauli ya ushirikiano huwezesha mhusika mmoja katika mawasiliano kuwasiliana kwa uchukulio kuwa mhusika wa pili anashirikiana vile vile. Kauli hii ya ushirikiano ina jukumu la kuelekeza yale tunayosema ili yaweze kuchangia katika malengo ya diskosi husika. Kwa upande mwingine, kauli ya upole ina jukumu la juu zaidi kuliko kauli ya ushirikiano kwani hudhibiti usawa na uhusiano mwema wa kijamii ambao hutuwezesha kuchukulia ya kuwa washirika wetu wanashirikiana nasi katika mawasiliano. Anaendelea kusema ya kuwa bila kuzingatia kauli ya upole, hatuwezi kuelewana na majirani wetu haswa tunapohitaji msaada wao.

Wakati mwingine, kauli ya upole huweza kuwekwa kando hasa wahusika katika mazungumzo wanapozungumzia suala ambalo ni la kuwahusu wote wawili na lililo na umuhimu kwao wote. Hata hivyo, kauli ya upole huchukuwa nafasi ya juu dhidi ya kauli ya ushirikiano hivi kwamba kauli ya ubora katika mazungumzo hupuuzwa. Hali kama hii hutokea pale ambapo mhusika mmoja analazimika kudanganya ili kujiokoa kutokana na hali fulani. Kwa mfano, unapoalikwa na mwandani wako katika sherehe fulani na ukajikuta kuwa hutaweza kuhudhuria sherehe kama hiyo, utalazimika kumdanganya kuwa utakuwa na shughuli nyingine wakati huo kwa hivyo hutaweza kufika katika sherehe hiyo ya rafiki yako. Mfano huu unalinganishwa na matamshi ya kinaya ambayo ufasiri wake huegemea katika kauli ya upole. Leech (1993) anarejelea mfano ufuatao:

*A*: *Geoff ameazima gari lako.*

*B*: *Naam, nafurahishwa na hayo*!

Katika mfano huo, kile *B* anasema ni upole kwa Geoff na si ukweli lakini kile ambacho *B* anamaanisha si ukweli kwani hajafurahishwa kamwe na hatua yake Geoff. Grice (1975) anaongezea kwa kusema ya kuwa mtu anayewasiliana kwa kinaya huonekana kumdanganya msikilizaji wake lakini huu ni uwongo ambao hawezi kuuepuka kamwe. Hali kama hii huweza kutokea wakati ambapo mhusika hawezi kusema ukweli. Mhusika akijipata ana marafiki wake ambao hawapaswi kumuona kama amekasirika, atatoa jawabu kama hilo alilotoa kwa mwenzake.

Grice (1975) anasema ya kwamba ukiukaji wa kauli hizi za mazungumzo husababisha kutokea kwa maana mbalimbali kwa usemi, jambo ambalo humfanya msikilizaji kutatizika kupata alichonuia mzungumzaji. Kwa mfano, mkulima atakayemwambia mwenzake:

*Ninahitaji soda baridi baada ya kufanya kazi juani.*

Jibu ambalo mwenzake atampa ni kwa mfano;

*Mkahawa uko nyuma yako.* (Tafsiri yangu)

Jibu hilo linatokana na mzungumzaji (mkulima), kuvunja kauli ya kiasi kwa kutotoa habari ya kutosha na hivyo basi kumfanya mwenzake kumjibu kwa namna alivyofikiria kuwa inaakisi maana iliyojitokeza katika usemi wa mkulima. Katika utafiti huu tulibaini jinsi kukosekana kwa habari kamili kuhusu uhifadhi wa misitu kutokana na matumizi ya mikakati mbalimbali ya kipragmatiki kunaifanya hadhira kutotekeleza jukumu la uhifadhi wa misitu namna ilivyotarajiwa.

Grice (1975) anasisitiza ya kuwa ufasaha wa kimaana unategemea kaida zilizoimarishwa na binadamu. Kwa mfano, mwanafunzi anayeinua mkono wakati mwalimu anauliza swali darasani, atachukuliwa ya kuwa analielewa jawabu litakikanalo. Mtaalamu huyu ameendeleza nadharia ya umaanishaji wa mazungumzo ambayo pasi na vitokanavyo na kile ambacho kimesemwa na watu, kuna pia kanuni zinazodhibiti mawasiliano; haya mawazo yanajaribu kuelezea kile ambacho kimechukuliwa kama vidokezi vya kimuktadha au

kiuamali. Kanuni hizi zinahusu mahusiano kati ya mawasilisho, maana yake, maana ya msemaji na vidokezi vyake. Grice (1975) anabainisha mwanzo, kile mtu husema na kile anachokidokeza. Matumizi ya kinaya kwa mfano, hudhihirisha hali ya kusema na kuelekea kusema. Mfano ufuatao unadhihirisha maelezo haya. Mzazi anayemwambia mwanaye aliyefanya kosa kuwa 'unanifurahisha sana na vitendo vyako!' anaelekea kusema kuwa hajafurahishwa na vitendo vyake huyo mtoto. Kwa mujibu wa Grice (1975) usemi kama huu unavunja kategria ya ubora wa mawasiliano kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 1.7 hapo juu. Habari iliyotolewa katika usemi huo si ya kina cha kutosha kumfahamisha msikilizaji ili kumuondolea utata wowote unaoweza kuzuka. Katika utafiti huu, tulichunguza utukiaji wa matumizi ya mikakati mbalimbali ya kipragmatiki kama vile kinaya katika diskosi za uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya na kueleza jinsi hali hiyo ilivyoelekea kutatiza kueleweka kwa moja kwa moja kwa habari ya mwandishi. Hali kama hiyo huweza kukatiza mawasiliano kati ya wahusika.

Kwa mujibu wa Grice (1975), umaanishi ni kihusishi kinachodokezwa na matamshi ya sentensi kimuktadha ingawaje wakati mwingine kihusishi hicho si sehemu ya kilichosemwa halisi. Kuna vimaanishi vya aina mbili: vimaanishi vya kaida ambavyo hutokana na vipashio vya maneno katika sentensi na vimaanishi vya mazungumzo ambavyo huainishwa katika makundi mawili yaani, maalumu na jumla. Vimaanishi maalumu hutokana na sifa asilia katika muktadha wa matamshi na kwamba sifa hizi hazibebwi katika sentensi iliyotumika. Kwa upande mwingine vimaanishi vya kijumla vinarejelea dhana kwamba matumizi ya mambo fulani ya maneno kwenye matamshi huweza kubeba kidokezo fulani cha maana. Katika umaanishi wa kikaida, kile ambacho kimedokezwa ni tofauti sana na kile kilichosemwa. Davis (1991) anarejelea mfano ufuatao: wahusika *A* na *B* wanazungumzia rafiki yao *C* anayefanya kazi kwenye banki. *A* anamwuliza *B* namna mwandani wao *C* anavyoendelea na kazi yake. *B* anajibu kwa kusema "ah vizuri sana, nadhani anawapenda wenzake na hajawahi kufungwa gerezani." Katika hali hii, *B* anadokeza jambo fulani - hajawahi kufungwa gerezani, ambalo *A* huenda akadadisi zaidi. Vidokezo kama hivi katika diskosi huweza kudokezea maana iliyodhamiriwa na msemaji iwapo vitafasiriwa vyema. Utafiti huu ulichunguza utukiaji wa vidokezo kama hivyo na kuona iwapo ufasiri wa umma wa habari juu ya uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo* uliathiriwa na vidokezo kama hivyo. Ukiukaji wa kategoria ya kiasi kwa mujibu wa Grice (1975) inamfanya msikilizaji au

msomaji wa habari kujaliza yaliyowachwa na mwandishi hali inayozua maana mbalimbali za tamshi. Hii ndiyo hali ambayo humfanya msomaji au msikilizaji wa habari fulani kujitokeza na fasiri zisizokamili hivyo basi kupotosha ujumbe ulionuiwa kuifikia hadhira. Utafiti huu ulichunguza jinsi ambavyo ukiukaji wa kategoria za mazungumzo huathiri ufasiri wa habari juu ya uhifadhi wa misitu nchini Kenya.

**1.8 Hitimisho**

Katika sura hii, vipengele takriban nane vimeshughulikiwa. Usuli wa utafiti huu ulionyesha mambo muhimu yaliyohitajika kama msingi wa kuhimili utafiti mzima. Suala la utafiti ambalo ndilo linalouelekeza utafiti huu lilibainishwa. Maswali ya utafiti pamoja na madhumuni yake yaliorodheshwa kikamilifu. Vilevile, mipaka ambayo utafiti huu ulitarajiwa kuzingatia pamoja na misingi ya uteuzi wa mada ya utafiti huu ilielezwa. Maelezo ya kina kuhusu umuhimu wa utafiti huu pamoja na nadharia iliyotumika katika utafiti wenyewe yalitolewa. Nadharia iliyotuongoza katika utafiti huu imezingatia kategoria nne ambazo ni muhimu sana katika utafiti wetu. Habari juu ya uhifadhi wa misitu inayokosa kuifahamisha hadhira vilivyo kwa kutoa habari chache au nyingi kupindukia itakuwa imekiuka kategoria ya kiasi. Hali kama hii hutatiza kueleweka kwa habari husika. Kwa upande mwingine, habari ambazo zinaonekana kuwa za uongo zitakuwa zimekiuka kategoria ya ubora. Aidha habari ambazo hazioani na mada husika- uhifadhi wa misitu, zitakuwa zimevunja kategoria ya kufungamana na mada. Hatimaye, habari ambazo huwa zimefumbwa kutokana na maelezo marefu kupindukia, au matumizi ya tamathali za usemi kama vile jazanda, methali miongoni mwa mifano mingine, zitakuwa zimevunja kategoria ya jinsi. Kwa hivyo, uvunjaji wa kauli hizo katika diskosi yoyote ile ya uhifadhi wa misitu huenda ukatatiza mawasiliano kati ya mwandishi na hadhira yake. Kategoria hizo zikizingatiwa katika mawasiliano yoyote yale, malengo ya mawasiliano hayo yatatimizwa bila utata. Katika utafiti huu, tulichunguza iwapo habari muhimu za kuhifadhi misitu zinazochapishwa katika gazeti la *Taifa Leo* hukosa kufasiriwa vilivyo na umma kutokana na kutozingatia kanuni zilizowasilishwa naye Grice (1975) hapo juu.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sehemu hii inatathmini maandishi mbalimbali yanayohusiana na pragmatiki na vilevile diskosi andishi ya uhifadhi wa misitu. Miongoni mwa maandishi yaliyorejelewa na kutathminiwa ni yale yanayohusiana na dhana ya pragmatiki ambapo maana ya dhana hii ilielezwa kwa uwazi. Tafiti mbalimbali za kipragmatiki na vile vile tafiti za uhifadhi wa mazingira hususan misitu zilirejelewa. Utata unaozuka katika juhudi za kujaribu kufasiri diskosi zilizozingatia mikakati mbalimbali ya kipragmatiki ulijitokeza na kujadiliwa. Mapitio hayo ya maandishi yanamweka mtafiti katika hali ya kuweza kuelewa jinsi wataalamu mbalimbali walivyolishughulikia suala zima linalohusiana na mada ya utafiti huu. Baadhi ya mbinu za kipragmatiki zilizojadiliwa katika sura hii ni pamoja na; kinaya, jazanda, umaanisho, methali na hatimaye matumizi ya uongo.

### 2.1.1 Dhana ya Pragmatiki

Kwa mujibu wa Shaozhong (2004), pragmatiki ni tawi la isimu lililochipuka mwisho mwisho mwa miaka ya sabini. Taaluma hii hujihusisha na uchunguzi wa jinsi ambavyo binadamu hufahamu na kutoa ishara ya kuwasiliana katika hali ya mazungumzo. Katika matamshi yoyote yale, taaluma hii hubainisha maana mbili: maana ya sentensi na maana ya mwasilishaji wa habari. Maana ya mwasilishaji wa habari ndiyo huzua utata kwani ufasiri utakaotolewa na msikilizaji au msomaji wa habari husika huenda usiwe ule uliodhamiriwa na mwasilishaji wa habari hiyo. Katika utafiti huu, fasiri mbalimbali za umma kuhusu diskosi andishi ya habari juu ya uhifadhi wa misitu nchini Kenya zilichanganuliwa ili kuonyesha jinsi ambavyo zilikosa kulenga dhamira ya mwandishi wa habari hizo kutokana na matumizi ya mikakati mbalimbali ya kipragmatiki katika diskosi husika.

Kwa upande wake, Kasper (1997), anasema ya kwamba ule uwezo wa kufahamu na kuweza kutoa ishara ya kuwasiliana hurejelewa kama umilisi wa kipragmatiki. Umilisi huu hujumuisha utambuzi wa tofauti za kijamii, mila za jamii mbalimbali na tofauti za kihadhi

kati ya mzungumzaji na wasikilizaji wake. Utafiti huu ulidhihirisha jinsi ambavyo hadhi ya wanajamii fulani kama vile wanasiasa huathiri fasiri za habari juu ya uhifadhi wa misitu na umma. Aidha, imani za kitamaduni kama vile ni lazima kuendelea kuishi mahali ambapo wazazi walizikwa zilidhihirika na kuathiri wahusika katika jinsi walivyofasiri habari za uhifadhi wa misitu na shughuli zinazohusiana na uhifadhi wa misitu kwa ujumla

Shaozhong (2004), amekuwa akijiuliza ni kwa nini wazungumzaji hufaulu kujadiliana katika mazungumzo yao. Shaozhong (2004), anasema ya kwamba ufanisi huu hutokana na wazungumzaji kuzingatia kanuni fulani. Kanuni ya kwanza wanayozingatia ni ushirikiano ambao huwawezesha wazungumzaji kuchangia katika mjadala wao. Kanuni ya pili ni upole. Kanuni hii ya upole huwawezesha wazungumzaji kuwa na heshima katika kujadiliana kwao. Kukosekana kwa kanuni hizi katika mazungumzo yoyote yale hukatiza mawasiliano. Katika utafiti wetu, fasiri za habari kuhusu uhifadhi wa misitu zilichunguzwa ili kubaini iwapo kanuni zozote zile za kipragmatiki ni miongoni mwa sababu zinazoathiri jinsi ambavyo wahusika hufasiri habari kuhusu uhifadhi wa misitu.

Hornby (2005), anatoa fasili ya pragmatiki kwa kusema kuwa ni uchunguzi wa jinsi lugha inavyotumiwa kuelezea kile mzungumzaji au mtu anamaanisha katika hali mahsusi haswa wakati ambapo maneno yaliyotumiwa huenda yakawa na maana tofauti kabisa. Maelezo haya ni muhimu katika kulitazama suala la matumizi ya semi mbalimbali pamoja na mbinu za lugha kama vile jazanda, kinaya miongoni mwa mbinu nyingine katika lugha. Katika matumizi ya mbinu hizo zote zilizotajwa hapo juu huwa na maana iliyotofauti na maneno yaliyotumiwa katika mbinu zenyewe. Katika utafiti huu, juhudi zilifanywa ili kubaini mikakati mbalimbali ya kipragmatiki kama vile jazanda, kinaya, matumizi ya methali au semi miongoni mwa mikakati mingine ambayo ilitumika katika diskosi zinazohusu uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo*. Uchunguzi ulifanywa ili kudhihirisha jinsi ambavyo mikakati hiyo huathiri jinsi ambavyo umma hufasiri habari zipatikanazo katika gazeti hilo la *Taifa Leo*.

Dhana ya pragmatiki vile vile imefasiliwa na wataalamu Bloomer, Griffiths & Merrison (2005) ambao kwa pamoja wanaelezea pragmatiki kuwa taaluma inayoshughulika na uchanganuzi wa lugha kimuktadha. Pragmatiki huangazia jinsi wazungumzaji au waandishi wa lugha wanavyotumia ufahamu wao kuwasilisha maana. Wataalamu hawa wanaendelea

kusema ya kuwa pragmatiki huchunguza jinsi lugha hutumiwa katika kufasiri matamshi au maandishi. Katika utafiti huu, uchunguzi wa mikakati mbalimbali ya kipragmatiki kama vile jazanda, umaanisho na kinaya ulifanywa ili kutambua jinsi ambavyo mikakati hiyo huathiri ufasiri wa habari kuhusu uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo*. Dondoo kutoka nakala za gazeti la *Taifa Leo* za baina ya mwaka wa 2008 na 2009 na zilizokuwa na habari kuhusu uhifadhi wa misitu ziliwasilishwa kwa umma ili wasome na watoe fasiri zao kuhusu habari hizo. Fasiri mbalimbali zilitolewa na wahojiwa kutegemea jinsi kila mmoja alivyoifahamu diskosi iliyowasilishwa kwake.

### 2.1.2 Tafiti za Kipragmatiki

Katika sehemu hii, kazi zilizoshughulikiwa kwa misingi ya pragmatiki na wataalamu mbalimbali zimerejelewa kwa lengo la kupata mwelekeo wa kushughulikia mada ya utafiti wetu-Ufasiri kipragmatiki wa diskosi andishi ya uhifadhi wa misitu nchini Kenya.

Indede (2009), anasema kuwa pragmatiki inajishughulisha na maana ya usemi; kile alichomaanisha msemaji wa usemi huo na jinsi usemi huo unavyofasiriwa na hadhira. Maana za kijuujuu za usemi ni za upekee hivi kwamba maana bwiwa huenda zisilete maana iliyonuiwa na mwandishi au msemaji wa usemi fulani kwani huenda zikatofautiana kabisa na kilichowasilishwa na maneno yaliyotumiwa katika usemi husika. Ili kufanikisha mawasiliano ya matini yoyote ile, uwezo na uwazaji wa maana iliyokusudiwa na msemaji au mwandishi wa matini husika pamoja na maana ya sentensi zilizotumiwa unahitajika. Mtaalamu huyo alirejelea diskosi za matamshi na maandishi ambayo ni ya kijumla kuhusu siasa. Vilevile, tumeelezwa jinsi ambavyo usemi wowote ule huweza kuwa na maana ambayo ni tofauti kabisa na kile kilichosemwa na mzungumzaji. Katika hali kama hii msikilizaji au msomaji wa matini husika huhitaji kufikiria kwa kina ili kupata fasiri kamili ya ujumbe ulionuiwa na msemaji. Utafiti huu ulijikita katika diskosi za maandishi pekee na haswa yanayochapishwa katika gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya juu ya uhifadhi wa misitu. Vile vile, mikakati ya kipragmatiki kama vile jazanda na semi/methali ilielezwa na kuonyesha jinsi ambavyo mikakati hiyo hubeba maana ya ndani iliyotofauti na ile ya nje ya mikakati yenyewe.

Aidha, mtaalamu Hofmann (1993), anasema ya kuwa wakati wowote lugha inapotumiwa, huwa kuna mzungumzaji na dhamira yake. Aghalabu dhamira yake huwa imefichika katika maana iliyowazi ya yale anayosema. Mianya kama hii kati ya maana iliyowazi ya sentensi na kile kinachowasilishwa hupatikana sana katika maisha yetu ya kila siku. Anaendelea kusema ya kuwa, katika matumizi ya sentensi zisizo na maana iliyowazi, wazo lililowasilishwa huwa si sawa na maana ya maneno katika hiyo sentensi. Hali kama hii hujitokeza waziwazi tunapotumia mbinu za lugha kama vile kupiga chuku, matumizi ya methali, kejeli, kinaya, matumizi ya tasfida na kadhalika. Hofmann (1993), anatambua kuwa mawasiliano ni ushirikiano kati ya mzungumzaji na anayezungumziwa. Anaendelea kuhoji kuwa lazima maneno yateuliwe vilivyo ili kusudi la mawasiliano lieleweke na pia anayezungumziwa aweze kufasiri yaliyokusudiwa na mzungumzaji. Utafiti huu ulichunguza iwapo palikuwapo na ushirika kati ya waandishi wa habari na wasomaji wa habari kuhusu uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo*. Aidha utafiti huu ulibaini kuwepo kwa baadhi ya mbinu za lugha zilizotajwa hapo juu na kwamba ziliathiri fasiri za habari za uhifadhi wa misitu.

Kwa upande mwingine, Habwe na Karanja (2004) wanasema ya kwamba wakati wa kuzungumza au kuandika, msemaji au mwandishi haelezi mambo fulani kwa uwazi. Hali hii inapelekea umaanishaji katika maana ambapo maana ambayo hutokeza siyo iliyozoeleka bali ni maana ya msemaji au mwandishi. Maana hii lazima ieleweke kwa sababu ya muktadha na elimu-shirikishi. Hali hii ya maana kadhaa kuweza kufasiriwa na msomaji wa matini fulani huweza kuzua utata wa kueleweka kwa ujumbe ambao mwandishi wa matini husika alidhamiria uifikie hadhira yake. Habwe na Karanja (2004) wametaja kutokea kwa fasiri mbalimbali za ujumbe ulioandikwa au kusemwa na mwandishi au msemaji. Katika utafiti huu, maelezo ya sababu za kutokea kwa fasiri hizo kadhaa yametolewa. Vile vile, mambo mahsusi yanayosababisha kutokea kwa fasiri mbalimbali za matini husika yameelezwa katika utafiti huu. Aidha wataalamu hawa wamerejelea mazungumzo kwa ujumla wala sio mazungumzo maalumu. Ili kuziba pengo hilo, utafiti huu ulijikita katika diskosi andishi pekee ambazo zinahusu uhifadhi wa misitu nchini Kenya na zinazopatikana katika gazeti la kila siku la *Taifa Leo*. Vilevile, utafiti huu uliweza kubaini mambo kama vile jazanda, umaanisho, kinaya miongoni mwa mengine ambayo husababisha utata katika kufasiri habari husika kama ilivyodhihirika kutokana na jinsi ambavyo umma ulivyotoa fasiri zao katika hojaji walizowasilishiwa.

Bloomer, Griffiths na Merrison (2005), wanasema ya kuwa katika kurejelea kauli ya Grice (1975) ya matendo ya ki-usemi yasiyo ya moja kwa moja, tamko la mzungumzaji huwa na maana nyingi isiyo ya moja kwa moja. Kwa mfano, tamko kama lifuatalo:

*Ninaweza kuzungumza lugha ya Kiswahili katika hotuba yangu?*

Tunapata maana kadhaa kutokana na tamko kama hilo. Mzungumzaji huenda ikawa anaomba ruhusa ya kuweza kutumia lugha ya Kiswahili au huenda ikawa anauliza hadhira yake iwapo inaelewa lugha ya Kiswahili ambayo angependa kutumia. Wataalamu hao wamechunguza maana mbalimbali zinazojitokeza katika mazungumzo mbalimbali ya kawaida hasa katika lugha ya Kiingereza. Larson & Segal (1998), wanasema ya kuwa ufahamu wa lugha hutoa tu maana ya kijumla ya tungo. Huwa kuna mwanya kati ya kile kilichosemwa na sentensi na kile ambacho mzungumzaji wa hiyo sentensi alinuia kuwasilisha kupitia hiyo sentensi. Huo mwanya huweza kuzibwa kwa kutumia pragmatiki ambapo maana kadhaa zinazojitokeza hufasiriwa vilivyo na kuamua maana iliyo na maantiki kwa msingi wa muktadha au mada husika. Utafiti huu ulichunguza maana mbalimbali zinazojitokeza kutokana na matumizi ya mikakati ya kipragmatiki katika habari kuhusu uhifadhi wa misitu zilizoandikwa katika gazeti la *Taifa Leo* nchini Kenya. Aidha, utafiti wetu ulibaini jinsi maana hizo kadha zinavyotatanisha kufasiriwa kwa habari hizo.

Lyons (1977), anasema ya kwamba ishara yoyote ile huwasiliana tu iwapo imedhamiriwa na anayeitoa kumfanya anayeipokea kufahamu jambo fulani ambalo hapo awali hakuwa amelifahamu. Kuwasiliana huko kunategemea jinsi ambavyo mtuma habari alivyochagua ishara za kuwasilisha ujumbe. Aghalabu huwa inachukuliwa kwamba ishara ambazo mtuma habari hutumia na ujumbe ambao mpokea habari hizo hupata huwa sawa. Lakini katika hali halisi huwa kunazuka kutowasiliana kwa sababu ya mpokea habari kutofasiri vilivyo ishara zilizotumiwa na mtuma habari. Kwa hivyo, ili mawasiliano yakamilike kwa njia iliyofaulu ni lazima anayepokea habari husika atambue dhamira ya mtuma habari hizo na vile vile afasiri habari hiyo kikamilifu kwa kutenda matendo yanayoashiria yale yaliyonuiwa na aliyetoa habari. Katika utafiti huu, uchunguzi ulifanywa ili kubaini iwapo matumizi ya mikakati ya kipragmatiki kama vile jazanda, kinaya, methali/semi na vivumishi yalikuwa na athari katika fasiri za habari kuhusu uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo*. Athari kama hizo huenda ikawa sababu ya kutofaulu kwa shughuli za uhifadhi wa misitu nchini Kenya.

Kwa upande mwingine, Davis (1991) anasema ya kwamba mzungumzaji au mwandishi huwasilisha ujumbe wake kupitia kile anachosema au kuandika kwa uchukulio kuwa msikilizaji au msomaji wake ataweza kufasiri kile ambacho mwandishi anatarajia atende. Hata hivyo, msomaji wa matini yoyote ile huweza kuzua maana tofauti tofauti kutegemea muktadha na imani yake. Masuala haya mawili, yaani muktadha na imani ya msomaji, huathiri jinsi anavyofasiri tamko lolote lile. Katika utafiti huu, dhana hizi mbili za muktadha na imani zilidhihirika kupitia diskosi za habari kuhusu uhifadhi wa misitu. Ilionekana waziwazi jinsi ambavyo fasiri mbalimbali kwa imani za kitamaduni zinavyoathiri kwa njia hasi juhudi za kuhifadhi misitu nchini Kenya. Baadhi ya fasiri hizo huwa potovu hivyo basi kutofaulisha mawasiliano baina ya mwandishi na msomaji wa makala husika.

Verschueren, Ola Ostman & Blommaert (1995), wanasema kuwa matumizi ya jazanda hayachukuliwi kuwa upotovu katika kusema ukweli katika maongezi yoyote yale ila ni hali ya kutafuta maana ya muktadha. Kufasiri kwa jazanda huhitaji juhudi fulani katika mifanyiko akilini kinyume na maongezi ya kawaida tu. Hata hivyo ni hadhira ambayo inatwikwa jukumu la kutafuta fasiri ya jazanda iliyotumika katika usemi husika. Katika hali kama hii, kuna uwezekano mkubwa wa msomaji au msikilizaji kujitokeza na fasiri isio sahihi ya usemi fulani. Fasiri kama hiyo huweza kupotosha ujumbe wa usemi wa mwandishi hivyo basi kutatiza mawasiliano. Katika utafiti huu, tuliweza kuchunguza jinsi ambavyo matumizi ya mikakati mbalimbali ya kipragmatiki kama vile jazanda katika diskosi ya uhifadhi wa misitu hupelekea hadhira kufasiri makala husika kwa njia isiyofaa na hivyo basi kutatiza mawasiliano.

Verschueren et al (1995) wanaendelea kusema ya kwamba, katika matumizi ya kinaya katika matini, wazo ambalo huwasilishwa huwa ni wakilisho la fikra za mzungumzaji mwenyewe. Ukweli wa mbinu ya kinaya huwa haupatikani katika maneno yaliyoandikwa bali ni katika mtazamo wa mwandishi kuhusiana na fikra iliyowasilishwa. Msomaji au hadhira kwa ujumla huwachiwa nafasi ya kuamua kile alichodhamiria mwandishi katika kutumia mbinu ya kinaya katika maandishi yake. Wakati mwingine msomaji huweza kuibuka na maana ambayo ni kinyume na aliyonuia mwandishi wa matini husika. Hali kama hii hutatiza mawasiliano kati ya mwandishi na msomaji kwa vile ujumbe alionuia mwandishi huwa haumfikii msomaji.

Aidha, Verschueren, Ola Ostman na Blommaert (1995) wanasema ya kuwa, kusema ya kwamba mwandishi fulani anatumia uchukulio wa miktadha ili kukisia ufasiri wa msomaji wa matini yake ni sawa na kusema kuwa hali kama hiyo huweza kutumiwa kama njia ya kukisia na kutarajia ufasiri wa msomaji. Hata hivyo, msomaji wa matini fulani hana idhibati kamili ya kutambua nia ya mwandishi wa matini husika. Kutokana na fasiri mbalimbali za matini husika na msomaji aliyelengwa na ambao huwa si sawa na ule ufasiri ulionuiwa na mwandishi, huwa kunatokea hali ya mawasiliano kutoafikiwa. Ni kutokana na misingi hiyo yake Verschueren na wenzake ndipo utafiti huu ulijikita katika kuchunguza athari zinazotokana na umma kufasiri diskosi zinazohusu habari za uhifadhi wa misitu kwa kuzingatia au kupuuza mikakati ya kipragmatiki.

Katika hali halisi, hakuna vidhibiti vyovyote vinavyomzuia msomaji wa matini fulani kuzidi kuongeza fasiri kadhaa katika matini husika hivyo basi kupata umaanisho tofauti tofauti wa matini hiyo. Wataalamu hawa wametuelezea uwezekano wa msomaji kupata fasiri mbalimbali kutokana na matini fulani. Hata hivyo, hawajatambua viambajengo vya kiisimu ambavyo husababisha hali kama hii ya kupata umaanisho tofauti tofauti kutokana na matini moja tu. Ili kuziba pengo hili, utafiti huu ulibaini mikakati mbalimbali ya kipragmatiki ambayo hutumiwa katika diskosi ya uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo* na kuonyesha jinsi ambavyo mikakati hiyo ya kipragmatiki husababisha kuzuka kwa fasiri mbalimbali ambapo ujumbe uliodhamiriwa na mwandishi hupotoka.

Kwa upande mwingine, Garnham (1985), anahoji kuwa madhumuni ya kimsingi ya lugha ni mawasiliano. Ingawa mawasiliano mengi huwa katika hali ya amri, maswali, nasaha au ahadi, matumizi ya lugha hudumu katika kueleza jinsi ulimwengu ulivyo. Uamilifu wa lugha ndiyo njia ya pekee inayodhihirisha uhusiano baina ya lugha na mawasiliano. Uwezo wa kufahamu lugha lazima udhihirishe namna ambavyo lugha hiyo inavyotenda kazi. Hata hivyo, uwezo wa kutumia lugha unaweza kuimarika au kudhoofika bila kubadili chochote katika ufahamu wa mtu. Katika utafiti huu, mbinu za kipragmatiki zilirejelewa katika kuchunguza jinsi ambavyo umma unavyofasiri habari kuhusu uhifadhi wa misitu. Katika hali hii, pragmatiki inaunganisha lugha na mawasiliano kwani mhusika anayetambua matumizi mbalimbali ya mikakati ya kipragmatiki anadhihirisha kiwango cha juu cha kuweza kufasiri

habari iliyowasilishwa kinyume na yule asiyekuwa na ufahamu wa mikakati hiyo ya kipragmatiki.

Utafiti uliofanywa naye Mulwale (2005), unaonyesha kuwa lugha hueleweka kwa kuzingatia muktadha mpana wa jinsi ilivyo kama njia muhimu ya mawasiliano. Umilisi wa kiisimu ni uwezo wa mtu kuzingatia kanuni zote za kimsingi zinazohusu lugha mahsusi. Uamilifu hutegemea umilisi wa kimawasiliano ambao hutokana na mifanyiko baina ya matukio ya kiakili na ile ya kijamii. Umilisi wa kimawasiliano hutumiwa na wanaisimu-jamii kurejelea uwezo wa msemaji katika kufahamu sheria za kisarufi, kileksia na kisemantiki pamoja na zile zitumiwazo katika miktadha maalumu katika jamii. Lugha hupenya katika mawanda yote ya maisha ya mwanadamu kiasi cha kufanya isiweze kutenganishwa na jamii. Kupitia lugha, watu hueleza matamanio yao, matarajio na wasiwasi wao kuhusu hali yao ya baadaye. Kujieleza huku hujitokeza kupitia lugha simulizi au andishi. Katika ufafanuzi wake, Mulwale (2005), anasisitiza ya kwamba uamilifu wa lugha huchangia katika kufasiri maana ya usemi au matini. Hata hivyo, mtaalamu huyu hajatueleza jinsi ambavyo pragmatiki huathiri kueleweka kwa maana katika matini husika. Katika utafiti huu, tulibaini namna ambavyo matumizi ya mikakati mbalimbali ya kipragmatiki inavyoathiri namna msomaji wa diskosi ya uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo* hufasiri ujumbe ambao alinuiwa aupate. Kwa mfano matumizi ya jazanda kama mkakati wa kipragmatiki katika diskosi ya uhifadhi wa misitu yaliwatatiza baadhi ya wasomaji wa diskosi hiyo. Wasomaji walipoulizwa kama wanakubaliana na hoja kuwa dhahabu inapatikana katika miti, wengine walipinga kauli hiyo (Rejelea H37, ukurasa wa 109). Fasiri kama hizi huweza kuwafanya wahusika kukosa kutambua umuhimu wa miti hivyo basi kutohifadhi misitu.

Aidha, Okombo & Habwe (2007), wamedhihirisha jinsi ambavyo matumizi ya vionyeshi katika lugha ya Kiswahili huweza kufasiriwa kwa njia tofauti tofauti na msikilizaji kinyume na hali halisi iliyodhamiriwa katika matumizi ya vionyeshi kama hivyo. Matumizi ya vionyeshi katika lugha ya Kiswahili ni mfano wa mikakati ya kipragmatiki ya kuwasilisha maana iliyonuiwa na mzungumzaji. Wawili hao wametoa mfano wa abiria wa gari la usafiri la *matatu* ambaye kwa kusema ya kwamba anaenda *hapa*, anaeleweka kumaanisha ya kuwa haendi mbali. Ukweli ni kwamba msafiri huyo alikuwa akienda mbali yaani Kawangware kutoka katikati mwa jiji la Nairobi. Umbali ulioko kati ya kitongoji cha Kawangware na

katikati mwa jiji la Nairobi si wa kurejelewa kuwa karibu. Matumizi ya kionyeshi *hapa* ni ya kipragmatiki ambayo yamenuiwa na mzungumzaji kupunguza umbali ulioko kati ya Kawangware na katikati mwa jiji la Nairobi ili asilipishwe nauli ya juu bali nauli ya kwenda *karibu*. Utafiti huu ulichunguza jinsi matumizi ya mikakati ya kipragmatiki miongoni mwao, vionyeshi na vimilikishi katika habari juu ya uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo* yanaathiri ufasiri wa ujumbe kama huo na hivyo basi kufanya shughuli za uhifadhi wa misitu nchini Kenya kutofaulu jinsi ilivyotarajiwa.

Indede (2009), anasema ya kwamba katika mawasiliano ya kisanaa, tunachukulia ya kwamba mbali na kuwa na matini husika, uwasilishaji na ufasiri wa matini kama hayo ni matendo ya kijamii. Ni muhimu kuchanganua mawasiliano ya kisanaa kwa ufahamu ili kuelewa malengo, mahitaji, matamanio na hata hisia za mwandishi. Matini yoyote ile humchochea msomaji kujenga taswira fulani ili kufanikisha ufasiri wake wa matini husika. Hali kama hii humchanganya msomaji kwani anaposoma shairi husika, mtunzi wa shairi kama hilo huwa hayuko karibu ili kumwelekeza katika ufasiri wake ambao huenda ukawa potovu. Msomaji kama huyo hulazimika kujitokeza na seti kadhaa za maana katika juhudi za kujaribu kupata fasiri iliyo sawasawa. Umaanishi wa kimuktadha huweza kuafikiwa na msomaji katika hali kama hii na hivyo basi kufanikisha mawasiliano yaliyonuiwa na mwandishi kumfikia msomaji wa kazi yake ya sanaa. Katika wasilisho lake, Indede (2009), alirejelea mawasiliano ya kisanaa. Vile vile alizungumzia utata unaozuka kuhusu ufasiri wa matini husika kwa kukosekana kwa mtunzi wa shairi husika wakati msomaji anapojaribu kulifasiri shairi hilo. Katika utafiti huu, tulijikita katika diskosi andishi ya kinathari ya uhifadhi wa misitu nchini Kenya ambayo hupatikana katika gazeti la *Taifa Leo*. Aidha, tulibaini mbinu kama vile jazanda, kinaya, umaanisho, vivumishi miongoni mwa mbinu nyingine zinazozua utata katika kufasiri diskosi husika hivyo basi kuathiri juhudi za kuhifadhi misitu nchni Kenya.

Kwa upande mwingine, Rahayu (2009), alifanya uchunguzi kuhusu matamshi ya ahadi ambayo yalitumiwa na Barrack Obama wa Marekani wakati wa kampeni yake ya kuwania urais mwaka wa 2008. Anatoa mfano mmoja wa tamko la ahadi alilotumia Obama- '*Nitapunguza ushuru kwa wafanyikazi.*' Rahayu anasema kuwa madhumuni ya kutoa matamshi ya ahadi kama hayo ni kuwapa mwitikio wasikilizaji. Hali kama hii ingewafanya waliomsikiliza Obama kuamua aidha kumpigia kura au kutompigia kutegemea jinsi

walivyoufasiri ujumbe kama huo. Kwa mfano, kwa sababu ya faida ambayo ingetokana na wao kumpigia Obama kura yaani kuongezewa mshahara, wanachukulia habari hii kuwa nzuri. Waliofasiri habari hii kumaanisha kuchangia katika kuzorotesha uchumi wa nchi ya Amerika, waliiona ahadi hiyo kuwa mbaya hivyo basi hawakumpigia Obama kura. Rahayu (2009), anaendelea kusema ya kwamba utafiti wake ulijaribu kutambua maana ya matamshi ya ahadi kwa misingi ya muktadha wa mzungumzaji. Obama alipotoa ahadi kama hii, lengo lake lilikuwa kupata kura za kumwezesha kufaulu katika uchaguzi wa urais nchini Marekani. Hii ni mojawapo ya fasiri ya wasikilizaji wa Obama katika kampeni zake. Fasiri mbalimbali za ujumbe mmoja kama huo wa Obama huweza kuzua maana tofauti tofauti hivyo basi kupotosha ujumbe ulionuiwa na mwandishi au mzungumzaji. Katika utafiti huu uchunguzi ulifanywa ili kubaini namna habari juu ya uhifadhi wa misitu inavyofasiriwa kwa njia tofauti tofauti na umma haswa kwa kuzingatia mikakati ya kipragmatiki na athari zinazotokana na fasiri za namna hiyo.

### 2.1.3 Kinaya

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), kinaya ni mbinu pana ambayo huchukua nafasi kubwa na hutoa mchango wake si katika mazungumzo tu bali pia katika utoaji wa mawazo yetu ya kila siku. Mbinu hii hutumiwa na waandishi ili kuiwezesha hadhira wafikirie kwa undani suala linaloongelewa ili waweze kupata ujumbe uliokusudiwa kufikishwa kwao. Mbinu hii ni mojawapo wa mbinu zinazotawala maongezi yetu hasa kutokana na uwezo wake wa kuficha hisia, maoni na mitazamo yetu sahihi. Sifa hii ya kinaya ya kuweza kuficha hisia, maoni na mitazamo ya mzungumzaji au mwandishi ndio iliyotuchochea kufanya uchunguzi wa kubaini iwapo matumizi yake huzua utata katika kufasiri makala juu ya uhifadhi wa misitu. Mfano uliotolewa naye Leech (1983), unadhihirisha maelezo hayo:

*A: Geoff ameazima gari lako.*

*B: Sawa, nafurahishwa na hayo*! (Tafsiri yangu)

Ni kinaya kwamba mhusika *B* anafurahishwa na habari za kuwa mwenzake ameliazima gari lake bila ruhusa yake. Hisia alizoficha mhusika huyo ni zile za hasira ingawaje hakutaka kuzionyesha au kuzisema kwa mwenzake. Kwa mujibu wa Leech (1983), mzungumzaji kama huyo hapo juu hukiuka kauli ya ushirikiano na kuzingatia kauli ya upole ili kumwachia msikilizaji kupata umaanishi wa maongezi yake. Katika utafiti huu, maelezo ya utukiaji wa mbinu kama hiyo ya kinaya katika diskosi juu ya uhifadhi wa misitu yalitolewa. Athari zinazotokana na fasiri za habari hizo kwa kutozingatia mkakati huo wa kinaya pia yalielezwa. Maelezo yaliyotolewa hapo juu yanadhihirisha jinsi mzungumzaji au mwandishi huweza kukiuka kauli ya ubora kwa kutumia kinaya. Mwandishi kama huyo humwacha msomaji wa habari zake akiwa katika hali ya kutoa fasiri ambayo huenda isiwe sahihi.

**2.1.4 Jazanda**

Kwa mujibu wa Nordquist (2012), jazanda ni lugha ya kitaswira ambapo ulinganisho wa vitu viwili visivyofanana hufanywa kwa kurejelea angalao sifa moja inayovileta vitu hivyo husika pamoja. Katika ulinganisho huu, kitu kisichojulikana huelezwa kwa kurejelea kile kinachojulikana. Nordquist (2012), anatoa mfano ufuatao ili kudhibitsha maelezo yake; *maisha ni safari*. Safari huwa na mwanzo na mwisho wake. Sifa hiyo ya kuwa na mwanzo na mwisho pia hupatikana katika maisha. Mtaalamu huyo aliamua kuvilinganisha vitu hivyo viwili kwa kuirejelea sifa hiyo.

Kwa upande wake, Davis (1991), anasema ya kuwa kufasiri jazanda yoyote ile kunategemea ushirikiano kati ya mwandishi au mzungumzaji na msomaji au msikilizaji. Kazi hii ya kufasiri jazanda kwa ujumla kunamhitaji mfasiri aweze kufikiria kwa makini ili afanikiwe kupata fasiri iliyosahihi. Kwa mujibu wa Davis (1991), hakuna sheria zilizowekwa za kuunda jazanda. Aidha hakuna maelezo yaliyochapishwa ya kufafanua aina mbalimbali za jazanda. Maana ya jazanda iliyotumiwa na mwandishi hufasiriwa na msomaji kulingana na kuelewa kwake kwa matumizi ya hiyo jazanda katika makala husika. Kutokana na maelezo hayo, ni dhahiri kuwa matumizi ya jazanda katika matini yoyote ile huzua maana mbalimbali ya matini husika. Msomaji atakayekumbana na jazanda iliyotumika katika makala fulani huenda akajitokeza na maana ambayo yeye kama msomaji huona kuwa inaakisi muktadha ambamo



MASENO UNIVERSITY

imetumika. Kwa mujibu wa Grice (1975), hali kama hii ya kutumia mbinu kama vile jazanda ambayo hufumba maana ya kilichoandikwa humnyima msomaji habari muhimu. Habari hiyo muhimu aliyonyimwa msomaji ndiyo ingemwezesha kuufasiri vilivyo ujumbe uliomo katika makala husika. Huku ni kukiuka kategoria ya Grice ya jinsi (kama ilivyoelezwa katika sehemu ya 1.7 uk. 8). Katika utafiti huu, matumizi ya jazanda katika diskosi juu ya uhifadhi wa misitu yalibainishwa. Maelezo yalitolewa na kuonyesha jinsi matumizi ya jazanda huweza kusababisha wasomaji wa makala husika kuibuka na maana mbalimbali ya usemi mmoja. Hali kama hii ndiyo huenda ikasababisha msomaji wa diskosi kama hiyo ya uhifadhi wa misitu kukosa kufasiri vilivyo ujumbe ambao ulinuiwa na mwandishi umfikie msomaji.

### 2.1.5 Umaanisho

Gazdar & Good, (1982) wanaeleza umaanisho kuwa ile hali ambapo tamko au sentensi iliyoandikwa hutoa maana iliyo tofauti kabisa na yale maneno ambayo yako katika sentensi hiyo. Hiyo maana iliyo tofauti kabisa na yale yaliyosemwa ndiyo huzua umaanisho wa yaliyosemwa jinsi ilivyoelezwa kwa undani katika sehemu ya 1.7, ukurasa wa 13. Kwa kudhihirisha maelezo hayo, Gazdar na Good walirejelea mfano ambapo mwalimu mmoja aliyetaka kujua jinsi mwanafunzi wake alivyokuwa akiendelea katika masomo yake ya uanafalsafa alimuuliza profesa katika taaluma hiyo ifuatavyo:

*Mwalimu: Mwanafunzi wangu anaendeleaje katika somo lake la falsafa?*

*Profesa: Mwandiko wake ni bora.* (Tafsiri yangu)

Umaanisho unaojitokeza katika tamko alilotoa profesa ni kuwa mwanafunzi huyo wa taaluma ya falsafa hajimudu katika somo hilo. Maana hiyo inayojitokeza kutokana na tamko lake profesa ni tofauti kabisa na maneno ambayo profesa aliyatumia katika tamko lake. Ili kuweza kufasiri tamko lililo na umaanisho, msomaji huhitajika kutafakari kwa makini kabisa ili kuweza kupata fasiri iliyosahihi. Aghalabu watu hujitokeza na fasiri tofauti tofauti kutokana na tamko moja ambapo baadhi ya fasiri hizo huwa si sahihi. Hali hii huweza kupotosha maana ya tamko lililowasilishwa na msemaji au mwandishi hivyo basi mawasiliano kukatika kati ya mwandishi na msomaji wake. Katika utafiti huu, fasiri

mbalimbali za umma kuhusu diskosi juu ya uhifadhi wa misitu ziliweza kubainishwa. Umaanisho uliojitokeza kutokana na matamshi mbalimbali katikia diskosi juu ya uhifadhi wa misitu ulielezwa na kuonyesha jinsi ambavyo kupotoka kwa ujumbe kulivyotokea. Hii ndio hali ambayo huenda ikawa hufanya wanaosoma diskosi juu ya uhifadhi wa misitu kukosa kutekeleza mambo wanayotarajiwa kufanya ili kuhifadhi misitu nchini Kenya.

Aidha, mfano ufuatao unadhihirisha jinsi ambavyo tamko moja laweza kuwa na maana kadha wa kadha kwa mujibu wa Bloomer, Griffiths na Merrison (2005)

*Kuna kipande cha samaki mezani.* (Tafsiri yangu)

Tamko hilo linaweza kuwa na maana zifuatazo:

1. Msemaji analalamika kuwa meza haijapanguzwa baada ya mlo wa samaki.
2. Onyo linatolewa kutomruhusu paka kuingia jikoni ili asile samaki.
3. Hakikisho kwa msikilizaji kuwa chakula cha siku hiyo kipo.
4. Msikilizaji anaalikwa mezani ili ale samaki.

Tamko hilo moja limeweza kuzua maana nyingi kiasi hicho kwa sababu msikilizaji amelifasiri tamko hilo kulingana na jinsi alivyolielewa. Tunaweza kusema ya kuwa huenda baadhi ya fasiri hizo si sahihi kwa mujibu wa mwandishi. Hali kama hii ndio huweza kuzua utata katika mawasiliano hivyo basi kukatiza mawasiliano baina ya mwandishi na msomaji wa yaliyoandikwa.

### 2.1.6 Methali

Kwa mujibu wa Lawal (1997), methali ni msemo mfupi ambao aghalabu hutumiwa kuelezea ukweli unaojulikana au jambo la kawaida. Methali huelezea undani wa jambo kwa njia ya ukweli na katika muktadha maalumu. Hali hii hutegemea ufahamu wa matukio mbalimbali katika mazingira yetu. Mtaalamu huyu alieleza vitendo vinavyotokana na matumizi ya misemo katika jamii ya Yoruba. Alichanganua muktadha wa kiisimu, kijamii pamoja na kisaikolojia ambao wasomaji na waandishi hutumia kwa umahiri ili kuweza kufasiri ujumbe

au maana ambayo hupatikana katika methali au misemo. Fasiri ya aina hii hufanywa kwa kuzingatia nadharia za kipragmatiki ambazo hujishughulisha na maana. Lawal anaongezea kuwa matumizi ya methali katika matamshi huchangia pakubwa katika kuathiri mawasiliano. Athari kama hizi katika mawasiliano ndizo huenda zikafanya msomaji wa ujumbe ulioandikwa akatoa fasiri ambazo si sahihi hivyo basi kupotosha ujumbe uliodhamiriwa na mwandishi. Lawal (1997) anatoa mfano ufuatao wa methali kutoka katika jamii ya Yoruba:

*Mtoto anawaye mikono ndiye hula na wazee.* (Tafsiri yangu)

Maana ya methali hiyo kwa mujibu wa Lawal ni kuwa mtoto ambaye ni nadhifu kitabia ndiye huweza kukaribishwa na wazee katika jamii yake ili ajumuike katika vikao vya wazee hao. Msomaji wa maandishi ambayo yatakuwa na matumizi ya methali kama hiyo atahitajika kutafakari ili aweze kuifasiri vyema. Fasiri iliyo sahihi pia itategemea ufahamu wa mhusika wa tamaduni na mazingira ya jamii husika la si hivyo, fasiri itakayotolewa itakuwa potovu. Katika utafiti huu, matumizi ya methali na misemo mbalimbali katika diskosi juu ya uhifadhi wa misitu ilibainishwa. Athari ya mbinu hiyo ya methali katika kufasiri habari iliyoandikiwa wasomaji wa gazeti la *Taifa Leo* vilevile ilielezwa.

### 2.1.7 Matumizi ya Uongo

Grice (1975), anasema ya kuwa, kila tunapozungumza, huwa tunachukulia ya kwamba washirki wote katika mazungumzo husika hujitahidi kufanikisha mawasiliano. Kwa hivyo inachukuliwa kwamba wahusika wote wana maelezo ya kutosha, wanasema ukweli, wanazingatia muktadha wa mazungumzo na kwamba wote wanaeleweka waziwazi. Hata hivyo hutokea wakati mwingine ambapo mzungumzaji husema uongo maksudi. Bloomer, Griffiths na Merrison (2005), wanatoa mfano ufuatao ili kudhihirisha matumizi ya uongo katika mazungumzo kwa nia fulani. Wanarejelea mtangazaji ambaye yuko katika studio za runinga akitangaza na kwamba kila baada ya muda mfupi angewaambia watazamaji wake kuwa:

*Mimi ni Rufus na nimelala kwa wakati huu.* (Tafsiri yangu)

Rufus alikuwa akisema uongo kwani alikuwa akiendelea na utangazaji wake katika runinga. Hakuna jinsi ambavyo mtu aliyelala angeendelea kutangaza. Rufus alidhamiria tu kuwachesha watazamaji wake na ndipo akaamua kusema uongo. Matumizi ya uongo katika mazungumzo au maandishi huwa na dhamira iliyofichika. Anayesoma habari kama hizo huhitajika kung`amua ujumbe uliofichika katika usemi kama huo ili aweze kupata maana iliyonuiwa na mwandishi. Katika utafiti huu, matumizi ya uongo katika diskosi juu ya uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo* yalibainishwa na maelezo kuhusu maana zilizojitokeza kutokana na matumizi hayo kutolewa. Fasiri kadhaa zinazojitokeza kutokana na matumizi ya mbinu hii ya uongo huweza kusababisha msomaji kutopata maana iliyodhamiriwa na mwandishi. Hali kama hii huenda ikawa ndio hufanya juhudi za kuhifadhi misitu nchini Kenya kutofaulu kwani wanaosoma habari kama hizo hukosa kupata habari kamili za kuwawezesha kutekeleza shughuli za uhifadhi wa misitu.

### 2.1.8 Tafiti za Uhifadhi wa Mazingira

Utambuzi wa umuhimu wa misitu umemfanya binadamu ajishughulishe na harakati mbali mbali ili kujaribu kuhifadhi misitu katika mazingira yake. Kupitia kwa njia za mawasiliano, habari za uhifadhi wa misitu zimeenezwa kote duniani ili kujaribu kuhifadhi misitu. Juhudi kama hizi za kiisimu za kuhifadhi misitu miongoni mwa nyinginezo zimeangaziwa katika sehemu hii.

Kiss (1990), anatambua umuhimu wa wenyeji wa sehemu yoyote ile katika kuhifadhi mazingira ya kiasilia. Anatoa mfano wa nchi ya Ghana ambapo wenyeji wa huko wamefaulu katika shughuli za uhifadhi wa mazingira yao asilia kwa kutumia imani zao za dini za Kiafrika. Anazidi kutoa mfano mwingine wa nchi ya Madagaska ambapo jamii mbili kuu katika nchi hiyo zinaishi katika hifadhi ya msitu wa Andohabela. Kwa kutumia imani za dini za Kiafrika ambazo hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa kutumia lugha, jamii hizo zimefaulu kuhifadhi mazingira yao kikamilifu. Wenyeji wa Ghana wameweza kutumia lugha vilivyo ili kupitisha ujumbe ambao umechangia katika kuhifadhi mazingira nchini mwao. Katika utafiti huu, mbinu mbalimbali za lugh zimebainishwa na kuelezwa jinsi zinavyoathiri mawasiliano baina ya waandishi na wasomaji wa habari juu ya uhifadhi wa

misitu nchini Kenya. Aidha, imani mbalimbali za kitamaduni zilidhihirika miongoni mwa umma. Imani kama hizo zilielezwa na kuonyesha jinsi zinavyoathiri wenyeji katika shughuli za kuhifadhi misitu nchini Kenya. Kwa mfano, baadhi ya wavamizi wa msitu wa Mau walidhihirisha imani kuwa hawawezi kuhama kutoka msituni na kuwacha makaburi ya babu zao. Imani kama hizi zinaendeleza uharibifu wa misitu nchini Kenya kwani kwa kukatalia msituni, wenyeji hao wataendeleza shughuli zao za kila siku za maisha msituni humo. Shughuli hizo ni kama vile ukataji miti kwa minajili ya kupata kuni, kupanda mazao yao na hata kuchunga mifugo yao.

Harrison (1996), anasema kuwa uharibifu wa misitu umeenea sana katika sehemu zilizo na idadi kubwa ya watu kama vile sehemu ya magharibi, mashariki na kusini mwa Afrika. Misitu ya Afrika Mashariki inaendelea kukatwa kwa kiwango cha kutisha cha asilimia nukta nane kwa mwaka. Uharibifu huu unaendelea licha ya juhudi kubwa za kuwafahamisha wenyeji wa sehemu hizo umuhimu wa kuhifadhi misitu. Harrison hajatueleza ni kwa nini wenyeji hawa hawaitikii mwito wa kuhifadhi misitu katika maeneo yao licha ya kuhimizwa na kukumbushwa kila mara. Hali kadhalika mtaalamu huyu amezungumzia uhifadhi wa misitu katika maeneo haswa ya Afrika Mashariki kwa ujumla. Pengo hili lilidhamiriwa kuzibwa na utafiti huu kwa kuchunguza mbinu za kipragmatiki zinazotumiwa katika habari za uhifadhi wa misitu na kubaini jinsi matumizi ya mbinu hizo yanavyotatiza kueleweka kwa ujumbe kuhusu uhifadhi wa misitu katika gazeti la kila siku la *Taifa Leo* nchini Kenya.

Kwa mujibu wa UNEP (1999), sababu za kijumla kuhusu kuzorota kwa hali ya mazingira si ukosefu wa ufahamu kuhusu madhara ya kimazingira yanayoukumba ulimwengu mzima bali ni ukosefu wa mawasiliano kati ya makundi mbalimbali yanayodhamini utatuzi wa matatizo hayo na wanaoathiriwa na matatizo hayo. Ripoti hii ya UNEP inatambua umuhimu wa mawasiliano katika kuhifadhi mazingira. Katika utafiti huu, suala la mawasiliano katika kupitisha ujumbe wa kuhifadhi misitu limepewa kipaumbele. Hata hivyo pengo lililoachwa kwa kutoeleza sababu za ukosefu wa mawasiliano hayo lilizibwa kwa kubaini mikakati mbalimbali ya kipragmatiki inayotumiwa katika diskosi juu ya uhifadhi wa misitu na kuonyesha jinsi mikakati hiyo huelekea kusababisha kukatika kwa mawasiliano kati ya waandishi wa habari kuhusu uhifadhi wa mazingira hususan misitu na wanaozisoma habari hizo- umma, hivyo basi kufanya jitihada za kuhifadhi misitu kutatizika.

Aidha, Toili (2000), anasema kuwa kwa manufaa ya wakazi wa mashinani, mwito wa kimazingira lazima ulenge katika kuwasilisha masuala yote kwa wanaolengwa pamoja na kuweka wazi matokeo na mapendekezo yanayotokana na shughuli hizi. Kwa kufanya hivyo, kanuni za mawasiliano, ushirika na usawa huimarisha usimamizi wa mazingira. Mchango wake Toili ni wa kupongezwa kwani amelipa suala la mawasiliano umuhimu katika kufanikisha juhudi za kuhifadhi mazingira hususan misitu. Hata hivyo, pengo alilowacha la kutoeleza kanuni za mawasiliano ambazo ni muhimu katika kufanikisha usimamizi wa mazingira lilizibwa na utafiti huu ambapo mikakati ya kipragmatiki ilibainishwa na kuonyesha jinsi inavyoathiri ufasiri wa habari juu ya uhifadhi wa misitu nchini Kenya.

Kwa upande wake, Mulwale (2005), anaeleza kuwa ukosefu wa mawasiliano ni kikwazo kikubwa katika uenezaji wa habari kuhusu uhifadhi wa mazingira miongoni mwa raia vijijini. Anaendelea kusema ya kwamba lugha hueleweka kwa kuzingatia muktadha mpana wa jinsi ilivyo kama njia muhimu ya mawasiliano. Umilisi wa kiisimu ni uwezo wa mtu kuzingatia kanuni zote za kimsingi zinazohusu lugha mahsusi. Uamilifu hutegemea umilisi wa kimawasiliano ambao hutokana na mifanyiko baina ya matukio ya kiakili na ile ya kijamii. Umilisi huu wa kimawasiliano hutumiwa na wanaisimu-jamii kurejelea uwezo wa msemaji katika kufahamu sheria za kisarufi, kileksia na kisemantiki pamoja na zile zitumiwazo katika miktadha maalumu katika jamii. Kupitia lugha, watu hueleza matamanio yao, matarajio na wasiwasi wao kuhusu hali yao ya baadaye. Mulwale anatambua kuwa umilisi wa lugha na isimu kwa ujumla humwezesha mhusika kuelewa na kufasiri ujumbe unaopatikana katika matini yoyote ile. Katika utafiti huu, uchanganuzi wa fasiri mbalimbali za umma kuhusu diskosi ya uhifadhi wa misitu ulifanywa ili kubaini njia mbalimbali ambazo hutumiwa na umma kufasiri habari juu ya uhifadhi wa misitu nchini Kenya. Aidha utafiti huu ulitambua kuwa kutumika kwa mikakati mbalimbali ya kipragmatiki katika diskosi kuhusu uhifadhi wa misitu ni sababu kuu ya kuitatiza umma katika kujaribu kufasiri habari hizo kikamilifu.

### 2.1.9 Hitimisho

Maandishi tuliyopitia katika sura hii yalihusu dhana ya pragmatiki pamoja na maelezo mbalimbali ya mikakati ya kipragmatiki inayotumika katika diskosi mbalimbali hususan

uhifadhi wa misitu. Wataalamu mbalimbali wamerejelewa na linalojitokeza ni kuwa pragmatiki huchunguza matumizi ya lugha kimuktadha. Aidha mikakati ya kipragmatiki ambayo hutumika katika diskosi mbalimbali hususan uhifadhi wa misitu zimebainishwa na kufafanuliwa. Imebainika wazi kuwa matumizi ya mikakati kama hiyo- jazanda, kinaya, methali/semi na matumizi ya uongo katika matini, huweza kuzua maana nyingine iliyotofauti na ile ya nje ya mikakati yenyewe. Suala la mawasiliano lilijitokeza kuwa muhimu sana katika kuwasilisha habari juu ya uhifadhi wa mazingira hususan misitu. Maandishi hayo kwa ujumla yameonyesha jinsi ambavyo fasiri za habari kwa misingi ya kipragmatiki zinavyotoa maana mbalimbali ambayo huweza kuleta utata katika kueleweka kwake. Hali kama hii huenda ikamtatiza msomaji au msikilizaji wa habari husika hivyo basi kumfanya asitende alichonuia mwandishi au msemaji wa habari hiyo.

# SURA YA TATU

# NJIA NA MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii, maelezo kuhusu utaratibu wa utafiti yametolewa. Muundo wa utafiti uliotumiwa katika utafiti huu umeelezwa kwanza ambapo muundo mseto wa kitathmini na kitakwimu ulizingatiwa katika utafiti huu. Mbali na muundo wa utafiti, vipengele vifuatavyo vimeelezwa: utafiti maktabani, utafiti wa nyanjani, mbinu za ukusanyaji data, uainishaji na mpangilio wa data na mwisho, uchanganuzi wa data. Utafiti maktabani ulihusisha kusoma na kuchanganua nakala za gazeti la *Taifa Leo* kwa lengo la kubaini mikakati mbalimbali ya kipragmatiki itumikayo katika diskosi ya uhifadhi wa misitu. Utafiti wa nyanjani ulijihusisha na kuupokeza umma-wakazi wa eneo la Msitu wa Kakamega, hojaji ili wajaze kwa lengo la kupata data ya fasiri ya umma ya habari juu ya uhifadhi wa misitu. Mbinu za kukusanya data zilijumuisha sampuli na usampulishaji data pamoja na uchanganuzi wa yaliyomo. Matumizi ya hojaji yalitusaidia kupata data kutoka kwa umma. Data iliyopatikana iliainishwa na kupangwa vilivyo tayari kwa uchanganuzi.

### 3.1.1 Mpangilio wa Utafiti

Utafiti huu ulizingatia muundo mseto wa utafiti ambapo muundo wa kitathmini na kitakwimu iliwianishwa. Muundo huu ulizingatiwa kwa kuwa humwezesha mtafiti kupata majibu mwafaka kwa maswali ya utafiti. Vile vile, maswali mengi ya utafiti huweza kujibiwa kwa ukamilifu (Johnson & Onwuegbuzie, 2004).

Utafiti huu ulitumia muundo wa utafiti wa kitathmini uliojumuisha maelezo ya fasiri mbali mbali ya wasomaji wa diskosi ya uhifadhi wa misitu. Strauss & Corbin (1990), wanatetea hoja kuwa utafiti wa kitathmini humsaidia mtafiti kuelewa namna matukio mbalimbali yanavyoathiriwa na hali halisi ya maisha. Kwa upande wao Johnson & Onwuegbuzie (2004), wanatoa hoja kuwa utafiti wa kitathmini ni bora kwa kuwa mtafiti anaweza kutumia tukio fulani kudhibitisha wazi wazi tukio lingine muhimu kwa wasomaji kupitia maelezo.

Muundo wa kitakwimu hutumiwa kuelewa tukio ambalo halijulikani. Aidha, husaidia katika upatikanaji wa ufahamu mpya ulio tofauti na hali inayojulikana (Strauss & Corbin, 1990). Muundo wa kitakwimu uliuwezesha utafiti huu kubaini kiwango cha utukiaji wa mikakati mbalimbali ya kipragmatiki katika matini zilizohusishwa katika utafiti huu na ambazo zinahusu uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo*. Matumizi ya vipimo vya asilimia yalidhihirisha utukiaji huo.

Tafiti zilizojishughulisha na uchanganuzi wa matini (Eggins 2004; Fairclough 2004) zilitumia uchanganuzi wa kitakwimu kutimiliza uchanganuzi wa kitathmini. Kwa hivyo, katika utafiti huu, uchanganuzi wa kitathmini ulitumiwa kama mbinu ya kueleza matokeo ya kitathmini huku uchanganuzi wa kitakwimu ukitumiwa kusisitiza vipimo pamoja na uhusiano wa vipengele vilivyokuwa vikitafitiwa (Rej. Jedwali 1 uk. 43 & Jedwali 2 uk. 52).

McLeod (2008), ameeleza umuhimu wa kutumia muundo mseto wa kitathmini na kitakwimu katika utafiti. McLeod (2008), anasema ya kuwa utafiti wa kitathmini hukusanya data ambayo haiko katika hali ya takwimu. Data ya aina hii ya kitathmini huwa ni ya maelezo na kwa hivyo huwa na changamoto katika uchanganuzi wake ikilinganishwa na ile ya kitakwimu. Hata hivyo, utafiti wa kitathmini huwa muhimu katika kuwatafitia watu binafsi haswa tunapotaka kujua kwa kina mitazamo na fikira za watu kama hao. Ni muhimu kutambua mitazamo na mambo wanayothamini watu tunapowatafitia. Mambo kama hayo hujumuisha muktadha wa utafiti kwa ujumla. Katika utafiti huu, tulichunguza jinsi ambavyo wasomaji wa habari kuhusu uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo* huweza kufasiri ujumbe ambao hupatikana katika diskosi hiyo. Utafiti huu ulibaini kuwa mitazamo na fikra za baadhi ya wasomaji wa diskosi juu ya uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo* iliwaathiri katika kufasiri kwao. Baadhi ya wahojiwa walishikilia kuwa kuhama kutoka misituni kulikozikwa baba zao ni jambo ambalo haliwezekani. (Rej. Data nambari 38, uk. 66).

Kwa upande mwingine, utafiti wa kijarabati hukusanya data katika hali ya takwimu. Data kama hiyo huweza kupangwa katika kategoria na kuorodheshwa katika viwango mbalimbali. Aidha data hiyo huweza kuwasilishwa katika majedwali ambayo hufanikisha kueleweka na vilevile kurahisisha uchanganuzi wake. Njia nyingine za utafiti kama vile uchunzaji na matumizi ya hojaji zinaweza kutupa data za kitathmini na kitakwimu. Kwa mfano, maswali funge katika hojaji huzua data ya kitakwimu ambayo huweza kuwekwa katika kategoria. Maswali kama vile

'ndio' au 'la' huweza kuwekwa katika kategoria na idadi ya majibu katika kila kategoria kuhesabiwa. Kwa upande mwingine, maswali wazi katika hojaji huzua data ya kitathmini kwani mhojiwa hutoa maelezo kama jibu lake kwa maswali.

Kutokana na maelezo hayo, muundo mseto uliochaguliwa katika utafiti huu ulifaa kwani kulikuwa na data ya kitakwimu pamoja na ya kitathmini. Utukiaji wa mikakati mbalimbali ya kipragmatiki katika diskosi ya uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo* ilihesabiwa na utukiaji huo kuwasilishwa kwenye majedwali. Aidha fasiri mbalimbali za wahojiwa kule nyanjani kuhusu masuala ya uhifadhi wa misitu zilijitokeza kimaelezo. Maelezo hayo ya wahojiwa yalichukuliwa kuwa data ya kitathmini. Hii ndiyo data iliyowasilishwa kwa uchanganuzi katika utafiti huu.

### 3.1.2 Utafiti Maktabani

Utafiti maktabani ulifanywa kwa kusoma, kuchunguza, kuchanganua, kuhakiki na kutathmini maandishi mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti. Azma ya kufanya hivyo ilikuwa kuchanganua kwa upana mada ya utafiti ili kuelewa namna mada hii ilivyoshughulikiwa na wataalamu mbalimbali. Maandishi yanayohusu nyanja ya pragmatiki pamoja na uhifadhi wa mazingira hususan misitu yalisomwa kwa kina na kutoa tathimini kwa minajili ya kuifanya mada ya utafiti kueleweka vyema. Aidha matoleo ya gazeti la *Taifa Leo* ya baina ya mwaka 2008 na 2009 yalikusanywa na kubainisha yale yaliyo na habari kuhusu uhifadhi wa misitu nchini Kenya. Nakala za magazeti kama haya zilichunguzwa ili kuteua yale yaliyoakisi mada ya utafiti ili yatumiwe katika utafiti huu. Gazeti la *Taifa Leo* liliteuliwa kutumiwa katika utafiti huu kwa sababu hili ni toleo la gazeti la kila siku ambalo hutumia lugha ya Kiswahili katika kuwasilisha habari zake. Aidha, lugha ya Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi katika nchi ya Kenya hivyo basi hueleweka na kutumika na watu wengi walio katika pembe zote za nchi na ambao ni wa viwango vyote yaani chini, wastani na juu. Wananchi wa viwango vya chini na wastani ambao aghalabu hutegemea sana kulima ili wapate kujikimu kimaisha na pia kutumia kuni kwa upishi ndio wanaolengwa sana katika shughuli za kuhifadhi misitu nchini Kenya.

### 3.1.3 Utafiti nyanjani

Jumla ya watu wazima hamsini (50) wanaojua kusoma na kuandika walijitokeza kushiriki katika utafiti huu. Hao washiriki kutoka katika mabaraza ya chifu walipewa dondoo kutoka katika nakala za magazeti ya *Taifa Leo* yaliyokuwa na habari juu ya uhifadhi wa misitu ili wasome na kutoa tathmini yao wakiongozwa na maswali katika hojaji iliyokuwa imeandaliwa na mtafiti. (Taz. kiambatisho1, uk. 80). Watu hao hamsini waliteuliwa kwa misingi ya uwezo wao wa kujua kusoma na kuandika. Aidha watu hao wote walikuwa wakazi wa eneo la msitu wa Kakamega hali ambayo iliwafanya kuwa na ufahamu wa dhana ya msitu. Ili kupata idadi hiyo ya watu 50 waliojitolea kuzijaza hojaji, ilibidi kuzuru mabaraza ya chifu takribani manne katika kata za Lukusi, Ivihiga, Kambiri na Lubao katika tarafa ya Ileho wilaya ya Kakamega Mashariki katika Kaunti ya Kakamega. Nilimtembelea kila chifu wa kila kata niliyozuru ili kupata wahojiwa. Niliwakabidhi hao machifu barua kutoka Chuo kikuu cha Maseno iliyonipa idhini ya kufanya utafiti wangu. Rej. Kiambatisho 3, uk. 124. Niliwaomba waniruhusu kuwakabidhi wananchi hojaji za kukusanya data ya utafiti wangu.

Kwa usaidizi wa hao machifu, nilijulishwa kwa wananchi ambao walikuwa wakihudhuria mikutano ya baraza la chifu. Nilipewa nafasi ya kuwahutubia wananchi hao na kuwaeleza nia yangu na vilevile kuwasihi kunisaidia kufanikisha kazi yangu ya utafiti. Niliwahakikishia ya kuwa utafiti wangu ulikuwa na nia nzuri ya kusaidia katika juhudi za serikali za kuhifadhi misitu nchini Kenya. Juhudi zangu za kuwatafuta wahojiwa hao zilifanikiwa kwani walijitokeza bila tatizo lolote. Nilichukuwa nafasi hiyo kuwashukuru iwapo wangenisaidia katika kufanikisha utafiti wangu.

Kwa ujumla niliweza kuwapata wahojiwa 50 ifuatavyo;

Kata ya Lubao, wahojiwa 15.

Kata ya Lukusi, wahojiwa 14.

Kata ya Ivihiga, wahojiwa 11.

Kata ya Kambiri, wahojiwa 10.

### 3.2.0 Mbinu za Kukusanya Data

Ukusanyaji wa data ulifanywa kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo pamoja na matumizi ya hojaji kwa kikundi lengwa.

### 3.2.1 Sampuli na Usampulishaji Data

Utafiti huu ulihusu uchanganuzi wa ufasiri kipragmatiki juu ya habari kuhusu uhifadhi wa misitu nchini Kenya. Mbali na Msitu wa Kakamega misitu mingine ambayo hupatikana nchini Kenya ni pamoja na Msitu wa Aberdares, Msitu wa Mlima Elgon, Msitu wa Mlima Kenya, Msitu wa vilima vya Cherengani pamoja na Msitu wa Mau. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999), asilimia kati ya kumi na thelathini (10%-30%) ya jumla ya watafitiwa wanaoweza kufikiwa na mtafiti inatosha katika utafiti wa kitathmini. Msitu wa Kakamega ni asilimia kumi na sita nukta sita 16.6% ya misitu yote mikuu sita nchini Kenya. Aidha, inachukuliwa kwamba matatizo yanayoikumba misitu hii yote haswa yanayohusu uhifadhi wa misitu ni sawa kwani misitu hiyo inapatikana nchini Kenya ambayo inaongozwa na serikali moja. Habari kuhusu uhifadhi wa misitu nchini Kenya na ambazo huchapishwa katika gazeti la *Taifa Leo* zilitumiwa kama sampuli ya kufanyia utafiti huu. Sampuli hii iliteuliwa kidhamirifu kutoka katika nakala za gazeti la *Taifa Leo* za baina ya mwaka wa 2008 na 2009. Kipindi hiki cha miaka miwili kilichukuliwa kwa sababu habari juu ya uhifadhi wa misitu huwa hazichapishwi kila siku bali ni baada ya muda usiotabiriwa. Kwa hivyo, kipindi hicho kilitupa idadi tosha ya nakala za magazeti ya *Taifa Leo* yaliyotumiwa kupata sampuli yetu. Jumla ya nakala zote thelathini na sita (36) zilizokuwa na diskosi ya uhifadhi wa misitu zilizopatikana kutoka katika gazeti la *Taifa Leo* baina ya mwaka wa 2008 na 2009 zilitumiwa katika uchanganuzi wetu.

Aidha sampuli ya wananchi kutoka katika eneo la Msitu wa Kakamega walipewa dondoo za diskosi juu ya uhifadhi wa misitu kutoka katika gazeti la *Taifa Leo* ili wasome na kutoa fasiri yao. Jumla ya wakazi hamsini (50) kutoka eneo hilo la Msitu wa Kakamega walijitokeza kushiriki katika utafiti huu. Wakazi hao wa eneo la Msitu wa Kakamega walitumiwa katika sampuli hii kwa sababu hao ni watu ambao walichukuliwa kuwa na ufahamu wa dhana ya msitu kutokana na kuishi kwao katika maeneo hayo tangu wakiwa watoto. Aidha, msitu huu

wa Kakamega ulifikika kwa urahisi na mtafiti ukilinganishwa na misitu mingine. Hali hii ilidhamiriwa kupunguza gharama ya utafiti huu. Idadi ya watu hamsini iliyotumiwa kutoka eneo hilo iliwakilisha umma ambayo husoma habari kuhusu uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo* na kutarajiwa kushiriki katika shughuli za uhifadhi wa misitu.

### 3.2.2 Uchanganuzi wa Yaliyomo

Utafiti huu ulihusu uchanganuzi wa ufasiri kipragmatiki juu ya habari kuhusu uhifadhi wa misitu nchini Kenya. Uchanganuzi wa yaliyomo ulifanyiwa nakala zote 36 za gazeti la *Taifa Leo* zilizokuwa na habari kuhusu uhifadhi wa misitu nchini Kenya. Sampuli hii iliteuliwa kidhamirifu kutoka kwa magazeti ya *Taifa Leo* ya baina ya mwaka wa 2008 na 2009. Kipindi hiki cha miaka miwili kilichukuliwa kwa sababu habari juu ya uhifadhi wa misitu huwa hazichapishwi kila siku bali ni baada ya muda usiotabiriwa. Aidha, wakati huo ulishuhudia migogoro mingi nchini Kenya kuhusu uhifadhi wa misitu hususan msitu wa Mau. Kwa hivyo, kipindi hicho kilitupa idadi ya kutosha ya nakala za gazeti la *Taifa Leo* zilizotumiwa kupata sampuli yetu. Jumla ya nakala zote thelathini na sita (36) zilizokuwa na habari juu ya uhifadhi wa misitu zilizopatikana kutoka katika gazeti la *Taifa Leo* baina ya mwaka wa 2008 na 2009 zilitumiwa katika uchanganuzi wetu. Uteuzi wa sampuli hii ulikuwa wa kidhamirifu ili kuondoa mapendeleo yoyote. Kulingana na mtaalamu Trochim (2006), katika usampulishaji wa aina hii ya kidhamirifu, huwa tunasampulisha tukiwa na dhamira fulani akilini. Huwa kwa kawaida tuna kikundi kimoja mahsusi au zaidi ambapo uamuzi huwa ushafanywa kishughulikiwe. Katika hali hii, nakala za gazeti la *Taifa Leo* zilizokuwa na habari kuhusu uhifadhi wa misitu zililengwa na utafiti huu.

### 3.2.3 Matumizi ya Hojaji

Jumla ya wananchi hamsini (50) kutoka katika mabaraza ya chifu katika eneo la Msitu wa Kakamega ambao waliteuliwa kwa misingi ya uwezo wao wa kusoma na kuandika walipewa hojaji iliyoundwa na mtafiti na ambayo ilikuwa na maswali ya kuwaongoza (Taz. kiambatisho1 uk.80). Wahojiwa hao walitoa tathmini yao kuhusu habari juu ya uhifadhi wa

misitu iliyokuwa katika nakala za gazeti la *Taifa Leo*. Kundi hili la wananchi liliwakilisha umma ambao hutarajiwa kusoma habari kama hizo juu ya uhifadhi wa misitu na baadaye kushiriki katika shughuli za kuhifadhi misitu nchini Kenya. Chombo hiki cha hojaji kilitumiwa kwa kukusanya data kwa sababu utafiti huu ulitarajia kupata data ambayo haingeweza kupatikana kutoka kwa umma kwa njia ya uchunzaji wa moja kwa moja. Kwa mujibu wa Touliatos & Compton (1988), data inayohusiana na maoni, mitazamo, hisia na kadhalika huweza kupatikana kupitia kwa njia ya hojaji. Hali ya wahojiwa kujua kusoma na kuandika pia ilipelekea mbinu ya kutumia hojaji kuwa mwafaka. Aidha, matumizi ya hojaji katika kukusanya data huokoa muda kwani data nyingi hukusanywa kwa muda mfupi.

Matumizi ya hojaji katika utafiti huu yalinuia kupata data juu ya ufasiri wa umma wa habari juu ya uhifadhi wa misitu. Vilevile, maoni ya umma juu ya shughuli za kuhifadhi misitu na athari zake, yaliweza kudhihirika kupitia matumizi ya hojaji. Kwa ujumla, matumizi ya hojaji yalituwezesha kutimiza lengo la kwanza na tatu katika utafiti huu.

### 3.3.1 Uainishaji na Mpangilio wa Data

Data katika utafiti huu ilipatikana kwa kutumia mbinu mbili za kukusanya data. Mbinu ya kwanza ilikuwa uchanganuzi wa yaliyomo nayo ya pili ikawa matumizi ya hojaji. Data iliyotokana na uchanganuzi wa yaliyomo iliwekwa katika kategoria tano: Umaanisho, kinaya, jazanda, methali/semi, matumizi ya uongo na mwisho, vivumishi (vionyeshi). Utukiaji wa mbinu hizo tano katika diskosi ya uhifadhi wa misitu katika nakala zote 36 za gazeti la *Taifa Leo* ulirekodiwa katika jedwali kwa kutumia ishara kama ifuatavyo: umaanisho-*um* jazanda-*jz*, kinaya-*kn*, methali/semi-*me/se*, uongo-*un* na vivumishi-*vi*.

Katika mbinu ya pili- matumizi ya hojaji, data iliyopatikana yaani majibu ya wahojiwa kuhusu habari za uhifadhi wa misitu iliweza kuwekwa katika kategoria tatu. Kategoria ya kwanza ilikuwa data iliyohusu mbinu ya umaanisho (um). Kategoria ya pili ilihusu data juu ya kinaya (kin) nayo kategoria ya tatu ikawa juu ya jazanda (jz). Kila kategoria ilipewa ishara ili data katika kategoria hiyo iweze kutambuliwa kwa hiyo ishara wakati wa uchanganuzi jinsi ilivyoonyeshwa hapo juu.

Kila fasiri iliyotolewa na mhojiwa ilichunguzwa na kulinganishwa na fasiri iliyotarajiwa kuwa sahihi kwa kurejelea nadharia iliyotumika katika utafiti huu yake Grice (1975). Alama za viwango vya kuwa sahihi zilitolewa. Alama ya 0-2 kwa alama tano ilichukuliwa kuwa chini ya wastani nayo alama ya 3-5 kwa alama zote tano, ilichukuliwa kuwa juu ya wastani. Matokeo hayo ya viwango vya kuwa sahihi kwa kila data katika kategoria hizo tatu yaliwasilishwa katika jedwali ili kutumiwa katika uchanganuzi. Mugenda na Mugenda (1999) anasema kuwa ili kuyapa majibu ya wahojiwa alama za viwango ambavyo vina umuhimu, ni lazima vibadala husika viwe vimewekwa katika viwango vya kimahusiano fulani. Hali hii hurahisishwa iwapo maswali yaliyoko kwenye hojaji ni maswalifunge. Katika utafiti huu, maswali yaliyoulizwa wahojiwa katika sehemu za A na B ya hojaji iliyotumiwa yalikuwa funge. Mhojiwa alihitaji kuchagua jawabu moja kati ya majibu matatu yaliyoulizwa. Majibu ya wahojiwa yaliwekwa katika viwango vya asilimia ili kurahisisha ulinganisho wa majibu hayo.

### 3.3.2 Uchanganuzi wa Data.

Kwanza, uchanganuzi wa yaliyomo ulifanywa ili kutambua kuwepo kwa mikakati ya kipragmatiki katika diskosi zilizoandikwa katika gazeti la *Taifa Leo* juu ya uhifadhi wa misitu nchini Kenya. Kila nakala ya gazeti la *Taifa Leo* iliyohusishwa katika utafiti huu, ilichanganuliwa ili kubaini aina mbalimbali za mikakati ya kipragmatiki zilizojitokeza. Utafiti huu ulitarajia kuwa kuwepo kwa idadi kubwa ya mikakati ya kipragmatiki na maana mbalimbali zilizojitokeza katika kila nakala ya gazeti la *Taifa Leo* kulidhihirisha kuwepo kwa utata mkubwa katika diskosi husika. Hali kama hii ndiyo huenda ikawa hutatiza kueleweka kwa ujumbe ambao huwa umedhamiriwa kuifikia hadhira. Data hii ilielezwa na tathmini kutolewa.

Hojaji zilizotolewa kwa kikundi wakilishi cha umma zilichanganuliwa kwa kubainisha maana kadhaa za kipragmatiki zilizofasiriwa na kila mhojiwa. Matokeo na maelezo kuhusu fasiri hizo yalitolewa na kuwasilishwa katika majedwali na hatimaye kujadiliwa ambapo ufafanuzi zaidi ulitolewa (Rej. uk. 43 & 52).

Aidha, fasiri mbalimbali zilizotolewa na kila mhojiwa zilihusishwa na shughuli za uhifadhi wa misitu. Tathmini ya fasiri hizo ilitolewa kwa njia ya kinathari. Kwa mujibu wa Luvaha (2009), uchanganuzi wa kitathmini husaidia katika ufahamu na utoaji wa maelezo ya kina kuhusu namna watu wanavyokumbana na hali halisi.

### 3.4 Hitimisho

Katika sura hii, muundo wa utafiti huu umefafanuliwa. Muundo mseto wa utafiti ulizingatiwa katika utafiti huu kwani data iliyokusanywa ilihitaji kuwasilishwa kwa njia ya kitakwimu pamoja na njia ya kitathmini. Utaratibu uliotumiwa katika kukusanya na kuchanganua data ili kukidhi madhumuni ya utafiti huu umeelezwa pia. Utafiti nyanjani pamoja na maktabani ulifanywa ili kuweza kupata data. Data kuhusu mikakati ya kipragmatiki katika diskosi ya uhifadhi wa misitu ilipatikana katika nakala za gazeti la *Taifa Leo* katika maktaba. Data hiyo ilipatikana kupitia mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo. Nayo data kuhusu fasiri mbalimbali za habari juu ya uhifadhi wa misitu iliibuliwa kutokana na hojaji zilizojazwa na umma nyanjani. Data iliyokusanywa kutoka nyanjani na maktabani iliweza kudhibitiwa kwa kuiweka katika kategoria tofauti tofauti kwa kurejelea mbinu za kipragmatiki- kinaya, jazanda, umaanisho, methali/semi, vivumishi na matumizi ya uongo- zilizobainishwa katika utafiti huu. Data hiyo hatimaye iliwasilishwa na kuchanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kitakwimu na kitathmini mtawalia.

# SURA YA NNE

# UASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Mjadala wa matokeo ya mikakati ya kipragmatiki katika diskosi ya uhifadhi wa misitu nchini Kenya pamoja na fasiri mbalimbali za umma zimeshughulikiwa katika sura hii. Matokeo hayo yamejadiliwa kwa misingi ya umaanisho, jazanda au utata, kinaya, methali au semi, uongo na matumizi ya vivumishi jinsi ilivyojadiliwa hapo awali katika sura ya pili. Utafiti wetu ulijishughulisha na madhumuni matatu yafuatayo: kubaini mikakati ya kipragmatiki inayotumiwa katika diskosi za uhifadhi wa misitu, kujadili mikakati ya kipragmatiki inayotumiwa na umma kufasiri maana katika habari juu ya uhifadhi wa misitu na mwisho, kueleza athari ya ufasiri wa kipragmatiki wa habari juu ya uhifadhi wa misitu kwa shughuli za uhifadhi wa misitu. Sura hii imegawika katika sehemu mbili: uchanganuzi wa data iliyotokana na diskosi ya uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo* na uchanganuzi wa data iliyotokana na mahojiano kupitia kwa hojaji zilizotolewa kwa umma na ambazo zilihusu habari kuhusu uhifadhi wa misitu nchini Kenya. Ingawaje uchanganuzi wa kimsingi umezingatia mbinu ya kitathmini, takwimu zimeweza kutumika ili kukadiria vipimo vya baadhi ya matokeo kwa kutumia viwango asilimia na idadi ya utukiaji. Aidha data zilizochanganuliwa ni zile zilizoelekea kutoa mchango wa haja katika utafiti huu kwa mujibu wa madhumuni yaliyotajwa hapo juu.

## 4.2.0 Mikakati ya Kipragmatiki katika Diskosi ya Uhifadhi wa Misitu

Data kuhusu mikakati mbalimbali ya kipragmatiki inayojitokeza katika diskosi ya uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo* imetolewa katika sehemu hii. Mifano ya mikakati ya kipragmatiki iliyotolewa ni kama vile; umaanisho (Um), matumizi ya jazanda (Jz), matumizi ya kinaya (Kin), matumizi ya vivumishi, methali/semi (Me/Se) na matumizi ya uongo (Un). Tazama jedwali 1, uk. 43.

**Jedwali 1: Utukiaji wa Mikakati ya Kipragmatiki**

| Mikakati ya Kipragmatiki | Idadi ya Utukiaji | Asilimia (%) |
|---|---|---|
| Umaanisho (Um) | 34 | 50.74 |
| Kinaya (Kin) | 17 | 25.37 |
| Jazanda (Jz) | 06 | 8.95 |
| Methali/Semi (Me/Se) | 07 | 10.44 |
| Vivumishi (V) | 02 | 2.98 |
| Uongo (Un) | 01 | 1.49 |
| **Jumla** | **67** | **100** |

### 4.2.1 Umaanisho

Kupitia kwa mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo, mikakati mbalimbali ya kipragmatiki iliweza kubainishwa kutokana na nakala za gazeti la *Taifa Leo* za baina ya mwaka wa 2008 na 2009 (Taz. kiambatisho 2T uk.112). Mojawapo wa mbinu hizo ni umaanisho. Mbinu hii ilijitokeza mara thelathini na nne, (50.74%) ya utukiaji wa mikakati yote sita iliyoshughulikiwa. Baadhi ya data iliyotambuliwa kudhihirisha umaanisho ni kama vile;

(1) *Wabunge hao walisema kuwa jamii kama zile za Ogiek zimezoea kuishi msituni na hazina mahali pengine pa kwenda.* (Rej. H1, uk. 79)

Kile ambacho wabunge hao wanasema ni kwamba jamii zinazoishi msituni haziwezi kuhama kutoka mahali humo. Usemi huo umezingatia kauli ya upole ili kudumisha utangamano. Kwa mujibu wa Leech (1983), bila kuzingatia kauli ya upole, hatuwezi kuelewana na majirani wetu haswa tunapohitaji msaada kutoka kwao. Hao wabunge wanafahamu ya kwamba wanahudumia raia walio chini ya serikali moja na hawangependa kuonekana kuhujumu serikali. Hata hivyo kwa kutoa kauli kama hiyo, watakaoisoma kauli hiyo watachukulia ya kwamba wabunge hao wanawaunga mkono waliovamia msitu. Juhudi za serikali kuzishawishi jamii kama hizo za *Ogiek* kuhama kutoka msituni ili msitu uweze kuhifadhiwa hazitafua dafu.

Bwana Hassan Noor aliyetwikwa jukumu la kuongoza kamati ya kushughulikia suala la msitu wa Mau alinukuliwa akisema hivi;

(2) *Taarifa imeshatolewa kuhusu jambo hili, kwa hivyo sitaki kuingiza taarifa zangu ndogo ndogo*. (Rej. T03, uk.123)

Usemi huu wa Bw. Noor umevunja kategoria ya kiasi. Kwa mujibu wa Grice (1975), mzungumzaji au mwandishi anahitajika kuyafanya maandishi yake yamfahamishe msomaji wake kadri iwezekanavyo. Bw. Noor anaposema, '...taarifa zangu ndogo ndogo', anamfanya msomaji wake kujiuliza ni taarifa gani hizo ndogo ndogo. Msomaji kama huyo atakuwa na fasiri mbali mbali kuhusu kile mwandishi alisema. Msomaji alitarajia msemaji kueleza kwa uwazi kile kilichotarajiwa kufanywa kuhusiana na shughuli za kuhifadhi msitu hasa ule wa Mau ili aweze kuamua ni mchango upi angetoa. Kwa kukiuka kategoria ya kiasi msemaji amemweka msomaji wake katika hali ya kuwa na fasiri mbalimbali ambapo baadhi yazo hazitatimiza lengo la mwandishi kuhusu uhifadhi wa misitu. Mwandishi amebana habari fulani muhimu ambayo laiti ingemfikia msomaji wake, huenda shughuli za kuhifadhi misitu zingefaulu moja kwa moja.

Data ifuatayo, (Rej. T9 uk. 115) inadhihirisha matumizi ya upole ili kudumisha ushirikiano.

(3) *Tunapanga kuwalipa fidia ya pesa au kuwapa mashamba mahali kwingine.*

Umaanisho unaojitokeza hapa ni kwamba hao maskwota wanapaswa kuondoka msituni kwa vyovyote vile. Kwa kuamua kutumia mkakati wa kipragmatiki wa upole, mwandishi anadhamiria kudumisha ushirikiano kutoka kwa maskwota. Kwa mujibu wa Leech (1983), kauli za upole na ushirikiano katika mazungumzo ni muhimu sana katika kufaulisha mawasiliano. Kauli ya upole hupunguza uhasama kati ya pande mbili husika katika mawasiliano hivyo basi kusababisha ushirikiano ambao hufaulisha mawasiliano.

Katika kuripoti kuhusu habari za waziri wa misitu, gazeti la *Taifa Leo* (Rej. T11 uk. 116) lilisema hivi;

(4) *Pia alieleza kuwa ana imani kufikia 2012 kiwango cha misitu nchini kitapanda kutoka 1.7% kama ilivyo sasa hadi 4% na kufikia kiwango kinachohitajika cha 10% mwaka 2030.*

Kutokana na data hii, umaanisho unaojitokeza hapa ni kuwa misitu nchini Kenya imeharibiwa kwa kiwango cha juu sana na kilicho cha kuhofisha. Kiwango cha kimataifa kinachokubalika kustawisha msitu ni 10% ilhali nchi ya Kenya imestawisha 1.7% pekee!

Katika matamshi yake waziri wa misitu, hatumuoni akizungumzia suala hili la uharibifu wa misitu kwa uzito unaostahili. Kile anachofanya ni kutumaini tu ya kwamba kiwango cha misitu nchini Kenya kitaimarika na kufikia 10% kufikia mwaka wa 2030. Waziri wa misitu amekiuka kauli ya kiasi kwani hajatoa maelezo ya kutosha kumfahamisha msomaji wa usemi wake ili aweze kufasiri ujumbe uliodhamiriwa kumfikia msomaji. Hali kama hii itawafanya wale wanaosoma habari kama hizo za waziri wa misitu kulichukulia suala la uhifadhi wa misitu kwa wepesi ilhali ni suala linalostahili kupewa uzito wa kutosha.

Katika T17, uk.118, kumenukuliwa matamshi yake Moi- rais mstaafu wa nchi ya Kenya akirejelea suala kuhusu uhifadhi wa msitu wa Mau ifuatavyo;

(5) *Niko na nyinyi na ninachunguza kwa makini jinsi serikali inalishughulikia suala la Mau.*

Kutokana na matamshi kama haya, umaanisho unaojitokeza ni kuwa rais mstaafu anawaunga mkono waliovamia msitu wa Mau na kwamba anawatia moyo kutotishika na kuondoka kutoka msituni kutokana na ilani iliyotolewa na serikali ikiwahitji kuuhama msitu huo. Ama kwa hakika uungwaji mkono wa aina hii haswa ikitiliwa maanani kuwa anayewaunga mkono ni mtu mashuhuri na mwenye hadhi kuu katika jamii huenda ukatatiza juhudi za serikali kujaribu kuhifadhi msitu wa Mau.

Mkakati wa kipragmatiki unaozua umaanisho umetumika katika data ifuatayo;

(6) *Kama serikali, naamini **tu**naweza kutafuta mbinu za kustawisha msitu huo*. (Rej. T36 uk. 121)

Matumizi ya kiambishi kinachorejelea nafsi ya kwanza katika wingi-*tu*, yanaleta maana ya kuwa washikadau wote katika suala zima la uhifadhi wa msitu wa Mau wameshirikishwa. Mnenaji wa usemi huu hajamtenga yeyote kutokana na suala la kutafutia suluhisho tatizo linaloukumba msitu wa Mau. Fasiri kama hii itawawezesha wahusika kuchukua jukumu la kuhifadhi msitu unaohusika. Hata hivyo, ufasiri utakaokuwa kinyume na huo wa hapo juu,

utawafanya wanaohusika kutochukua hatua mwafaka za kuhifadhi msitu huo jambo ambalo litatatiza juhudi za serikali za kuhimiza wananchi kuhifadhi misitu nchini Kenya.

Matamshi yafuatayo kutoka katika T34, (uk. 120), yanazidi kudhihirisha umaanisho unaojitokeza kutokana na usemi mbalimbali ambapo fasiri mbalimbali hutolewa na msomaji jambo ambalo huleta utata katika maana iliyodhamiriwa na mwandishi.

(7) *Baadhi ya maskwota wamekuwa wakiishi katika maeneo ya msitu huo kwa zaidi ya miaka 50.*

Muda wa nusu karne ni mrefu sana ambapo kumtaka mtu ahame mahali ambapo amepajua kama nyumbani kwake ni kama kumdhulumu. Ujumbe unaotokana na nukuu hiyo ni kuwa maskwota hao hawawezi kuhama kutoka msituni kwani hapo ndipo nyumbani kwao. Katika hali kama hii, maskwota ambao watatarajiwa kusoma habari kama hiyo na watarajiwe kushiriki vikamilifu katika juhudi za kuhifadhi misitu watafanya kinyume kwani wataona kwamba wanaungwa mkono kuendelea kuishi ndani ya msitu husika. Kwa mujibu wa Hofmann (1993), mawasiliano ni ushirikiano kati ya mzungumzaji na mzungumziwa. Lazima maneno yateuliwe vilivyo ili kusudi la mawasiliano lieleweke na pia anayezungumziwa aweze kufasiri yaliyokusudiwa na mzungumzaji. Kutokana na jinsi habari hiyo katika T34 ilivyowasilishwa kwa msomaji, ujumbe utakaopatikana na msomaji wake sio ule unaotarajiwa kusaidia katika juhudi za kuhifadhi misitu.

### 4.2.2 Jazanda

Mbinu ya jazanda ilijitokeza mara sita, (8.95%) ya utukiaji wa mikakati yote sita ya kipragmatiki katika nakala za gazeti la *Taifa Leo* zilizoshirikishwa katika utafiti huu. Katika mfano ufuatao, mwandishi ametumia jazanda katika maelezo yake na katika kufanya hivyo, amefumba ujumbe ambao msomaji anatarajiwa kupata.

(8) ... *wakulima wengi wameonelea kuwa wanaweza kusaidia <u>gurudumu hilo</u> kwa kuanza kupanda miti.* (Rej. T26, uk.119).

Haikuwa nia ya mwandishi wa habari hiyo kuufumba ujumbe wake bali kutumia mbinu ya lugha inayoonyesha weledi wa lugha yake. Msomaji wa habari kama hiyo atatatizika

kujaribu kung'amua maana ya jazanda iliyotumiwa katika usemi huo. Kile mwandishi anamaanisha hapa ni kuwa wakulima wasaidie katika harakati za kuhifadhi misitu. Matumizi ya mikakati ya kipragmatiki kama hii katika diskosi yoyote ile ya uhifadhi wa misitu huweza kuzua utata katika kufasirika kwake hivyo basi kufanya madhumuni ya serikali ya kuhifadhi misitu kutofaulu. Katika hali kama hii, mwandishi anahitajika kufafanua zaidi usemi wake ili msomaji aweze kupata ujumbe wake moja kwa moja. Kwa kubana habari kwa msomaji kupitia matumizi ya jazanda, kile alichofanya mwandishi ni kukiuka kategoria za kiasi na jinsi kwa mujibu wa Grice (1975).

Tunaporejelea nakala ya T5, (uk.113), nukuu ifuatayo inadhihirisha matumizi ya jazanda ambapo matumizi yake yanazua fasiri mbalimbali.

(9) *Hayo ni machozi ya mamba tu.*

Umaanisho unaojitokeza hapa ni kwamba wale wanaojifanya kuwalilia wale waliofurushwa kutoka katika msitu wa Mau wanawahadaa tu hao maskwota kwa sababu hao wabunge walishiriki katika kupitishwa kwa hoja ya kuwafurusha maskwota kutoka katika msitu huo wa Mau. Maelezo hayo ya msemaji hayajajieleza wazi wazi kuhusiana na suala linalorejelewa kuhusiana na uhifadhi wa msitu wa Mau. Kwa kufanya hivyo, kategoria ya kiasi imekiukwa na hivyo basi kuwafanya wasomaji wa habari hiyo kuwa na fasiri tofauti tofauti. Baadhi ya wasomaje wake hawataelewa maana ya jazanda hiyo na hivyo basi kushindwa kufasiri ujumbe ulionuiwa umfikie msomaji wake. Vile vile, kauli ya jinsi imêkiukwa ambapo kwa mujibu wa Bloomer (2005), mzungumzaji hapaswi kuyafumba matamshi yake kiasi cha kumfanya msikilizaji wake kushindwa kupata ujumbe ulionuiwa. Ufumbaji wa habari yoyote ile humfanya msomaji kujitokeza na fasiri mbalimbali ambapo baadhi yake huwa potovu.

### 4.2.3 Kinaya

Jinsi ilivyoelezwa katika sehemu ya mapitio ya maandishi, matumizi ya kinaya katika matini yoyote ile huweza kuzua maana mbalimbali. Maana kama hizo humhitaji msomaji kuweza kutafakari vilivyo ili kupata fasiri iliyosahihi. Matumizi ya kinaya katika nakala za gazeti la *Taifa Leo* yalijitokeza mara kumi na saba, hii ilikuwa asilimia ishirini na tano nukta tatu saba

ya utukiaji wa mikakati yote sita iliyochunguzwa katika utafiti huu. Katika kiambatisho cha T1, (uk. 112), kuna matamshi yafuatayo ambayo yamenukuliwa na ambayo yanadhihirisha matumizi ya kinaya ambapo maana ya usemi huo unazua utata katika kufasiriwa kwake.

(10) *Waziri mkuu amekuwa akishutumiwa na baadhi ya wanasiasa kwa kuongoza juhudi za kuwaondoa walowezi waliovamia msitu wa Mau.*

Wabunge kama viongozi wa wananchi wanatarajiwa kuunga juhudi za serikali za kuimarisha mazingira ya raia wake. Suala la kuhifadhi msitu kama ule wa Mau ni la umuhimu mkubwa. Ni kinaya kuwasikia baadhi ya wanasiasa wakipinga juhudi kama hizo. Hali kama hii huwafanya wananchi kuchukulia kwamba shughuli kama hizo za kuhifadhi msitu si za umuhimu mkubwa hivyo basi kuzipuuza.

Vilevile, nukuu ifuatayo ya mwanasiasa mmoja inadhihirisha jinsi matumizi ya mbinu ya kinaya huzua utata katika kufasiri habari husika.

(11) *Viongozi wa Kanu mkoani Rift Valley wameiomba serikali iondoe marufuku ya kutotumia ardhi iliyo karibu na Msitu wa Mau ili wananchi warejelee shughuli za kawaida za kilimo.*

Huku ikitarajiwa kuwa viongozi wa umma wanastahili kuwashauri wananchi vilivyo kuhusu shughuli za uhifadhi wa misitu, viongozi walionukuliwa katika dondoo hili wanaelekea kuwaeleza wananchi wao kwamba wanastahili kujihusisha na shughuli za ukulima katika maeneo ya misitu. Hali kama hii ndio hutatiza juhudi za serikali za kuhimiza wananchi kuhifadhi misitu nchini Kenya.

### 4.2.4 Vivumishi

Matumizi ya vivumishi haswa vivumishi vimilikishi katika diskosi huzua mikakati ya kipragmatiki. Mikakati kama hiyo huathiri mawasiliano kwani huhitaji fasiri sahihi ili kufanikiwa kupitisha ujumbe ulionuiwa na mwandishi. Mkakati huu wa kipragmatiki ulitukia mara mbili katika nakala zote 36 za gazeti la *Taifa Leo* zilizotumiwa katika utafiti huu. Hii ilikuwa asilimia 2.98 ya utukiaji wa mikakati yote sita ya kipragmatiki. Katika data ifuatayo, matumizi ya kivumishi kimilikishi yamedhihirishwa.

(12) *Naomba viongozi wa dini muwaombee wanasiasa **wenu**.* (T05, uk. 113)

Ni wazi kuwa Bw. Sirma ni mmoja wa wanasiasa wa mkoa wa Bonde la Ufa ambaye anaunga mkono shughuli za kuhifadhi msitu wa Mau. Katika matamshi yake, mwanasiasa huyo ametumia kivumishi kimilikishi-*wenu.* Kivumishi hiki kinaleta dhana ya utengano. Mwanasiasa huyo amejitenga na wanasiasa wenzake ambao wamekuwa wakihujumu juhudi za kuhifadhi msitu wa Mau kwa visingizio mbalimbali. Kwa kutumia tu kivumishi hiki bila kueleza wazi wazi hila za wanasiasa wenzake kuhusiana na suala zima la msitu wa Mau, msemaji amewanyima wasomaji wa habari yake ujumbe muhimu ambao ungewawezesha kupata ufasiri kamili wa aliyosema. Kwa ujumla umaanisho wa matamshi yake msemaji ni kuwa hao wanasiasa wapinzani wana dosari kwani lile wanalopinga-kuhamishwa kwa maskwota kutoka msitu wa Mau, ni suala ambalo lilifaa kutekelezwa ili msitu wa Mau uhifadhiwe kwa manufaa ya jamii nzima ya Kenya. Mwanasiasa huyo anapowakabili wanasiasa wenzake ambao wanalipinga suala la kuwahamisha maskwota kutoka katika msitu wa Mau, kile anachomaanisha ni kuwa wanasiasa hao wabishi wana makosa ambayo yanahitaji nguvu zake Mungu ili waweze kujirekebisha na kubadili msimamo wao. Msemaji hajayasema haya kwa njia iliyo wazi. Hali kama hii humfanya msomaji wa makala kama hayo kutoa fasiri isiyokuwa sahihi kwa mujibu wa mwandishi.

**4.2.5 Uongo**

Mwandishi yeyote anapotumia mbinu ya uongo, huwa anafanya hivyo kwa lengo fulani lilofichika. Hii ni mbinu ya kipragmatiki ambayo humhitaji msomaji kufikiria kwa kina ili aweze kung'amua lengo lililofichika la mwandishi. Data ifuatayo inadhihirisha matumizi ya uongo.

(13) *Mvua hutoka juu, mvua haitoki kwenye miti.* (Rej. T7, uk. 114)

Matamshi kama haya yaliyotolewa na mwanasiasa Paul Sang ni ya uongo. Mwanasiasa huyo anafahamu fika kwamba mvua husababishwa na kuwepo kwa miti ilhali yeye anasema kinyume akiwa na lengo la kisiasa-kuwafurahisha maskwota waliokuwa wamefurushwa kutoka katika msitu wa Mau. Mwanasiasa huyo angependa maskwota hao waonekane

kutokuwa na makosa kwa kuuvamia msitu wa Mau. Pia ionekane ya kwamba lawama zinazozidi kutolewa kwamba uvamizi huo wa msitu wa Mau ndio chanzo cha ukosefu wa mvua nchini hazina msingi. Tukiyachunguza matamshi yake huyu mwanasiasa, tunapata kuwa kategoria ya ubora katika mazungumzo imekiukwa. Kwa mujibu wa Grundy (2000), mzungumzaji anahimizwa kutosema kile anachoamini kuwa ni uongo. Walowezi wa msitu wa Mau wanapozisoma habari kama hizi bila shaka hawataona kama kuna umuhimu wa kuhifadhi msitu wowote ule haswa ule wa Mau na hii ni kwa sababu ya ufasiri potovu utakaotokana na matamshi ya mwanasiasa kama huyo aliyerejelewa. Hali hii ya kutosema ukweli ilijitokeza mara moja katika nakala zote 36 za gazeti la *Taifa Leo* zilizotumiwa katika utafiti huu. Hii iliwakilisha asilimia 1.49 ya utukiaji wote wa mikakati sita ya kipragmatiki iliyochunguzwa.

### 4.2.6 Methali/Semi

Methali na semi hutumiwa na waandishi ili kuelezea undani wa jambo fulani kwa kurejelea ukweli unaojulikana. Katika kiambatisho T26, uk.119, mwandishi ametumia semi ifuatayo;

(14) *Huku serikali inapoendelea kupigia debe upandaji miti ili kuhifadhi mazingira na kuwaadhibu wale wanaokata miti katika misitu...kupanda miti.*

Semi iliyotumika katika dondoo hili ina maana kwamba serikali inahimiza upandaji miti kwa minajili ya kuhifadhi mazingira. Kwa msomaji asiye na ufahamu wa semi kama hii itakuwa vigumu sana kwake kutimiza mahitaji ya serikali ya kuhifadhi misitu kwani hataelewa habari itakayokuwa imechapishwa. Kwa mujibu wa Lyons (1977), ishara yoyote ile huwasiliana tu iwapo imedhamiriwa na anayeitoa kumfanya anayeipokea kufahamu jambo fulani ambalo hapo awali hakuwa amelifahamu. Matumizi ya semi zisizofahamika na msomaji humfanya msomaji kushindwa kufasiri habari kuhusu uhifadhi wa misitu inavyohitajika hivyo basi kutotekeleza shughuli za kuhifadhi misitu. Katika dondoo lililonukuliwa hapo juu, mwandishi amevunja kauli ya jinsi. Kwa mujibu wa Grice (1975), mwandishi anapaswa kutofumba maandishi yake ili yasizue utata katika kufahamika kwake. Semi iliyotumika katika maandishi ya hapo juu inasababisha utata katika kufasirika kwa maandishi hayo hivyo basi kukosa kuwasilisha ujumbe ulionuiwa na mwandishi.

Nukuu ifuatayo kutoka katika nakala ya gazeti la *Taifa Leo*, (Rej. T15, uk.117), vilevile inadhihirisha matumizi ya methali.

(15) *Waziri huyu wa kilimo aliyekolea ubishi akaamua baniani mbaya kiatu chake ni dawa.*

Matumizi ya mbinu kama hiyo ya methali huzua utata katika kueleweka kwa habari kwani inambidi msomaji kutafakari kuhusu maana ya methali husika kwanza kabla ya kuweza kufasiri kile alichomaanisha mwandishi wa habari husika. Mwandishi anayetumia mbinu kama hii katika uandishi wake huwa amekiuka kauli ya jinsi ambayo humhitaji mwandishi kutofumba mazungumzo yake na asizue utata katika mazungumzo yake ili ujumbe wake ueleweke bila kutatiza anayeupokea. Maana ya methali hii ni kuwa mtu aliye mbaya kwako huwa angalau na chembechembe fulani za uzuri ambazo unaweza kuzitumia kwa manufaa yako. Msomaji ambaye haelewi maana ya methali hii itamuia vigumu sana kuweza kupata ujumbe wa mwandishi wa habari husika. Hali kama hii huenda ikatatiza wasomaji wa habari za uhifadhi wa misitu zinazopatikana katika gazeti la *Taifa Leo*. Mbinu hii ya methali ilitukia mara saba katika nakala zote thelathini na sita zilizohusihwa katika uchunguzi huu. Hii iliwakilisha asilimia 10.44 ya utukiaji wa mikakati yote sita iliyotambuliwa.

**4.2.7 Muhtasari**

Jumla ya mikakati sita ya kipragmatiki iliweza kubainika katika nakala zote thelathini na sita (36) za gazeti la *Taifa Leo* zilizohusishwa katika utafiti huu. Utukiaji wa mikakati hiyo ya kipragmatiki katika diskosi ya uhifadhi wa misitu katika nakala zote 36 za gazeti la *Taifa Leo* uliweza kudhihirika jinsi ilivyowasilishwa katika jedwali la kwanza katika ukurasa wa 53. Utukiaji wa mbinu ya umaanisho ilichukuwa asilimia hamsini nukta saba nne (50.74%). Hii ilikuwa asilimia ya juu zaidi ya mbinu zote. Mbinu ya kinaya nayo ilichukuwa nafasi ya pili kwa asilimia ishirini na tano nukta tatu saba (25.37%) ya jumla ya utukiaji wa mikakati yote iliyohusishwa. Mbinu zilizosalia zilikuwa za asilimia ya chini. (Rej. jedwali1, uk. 43). Kwa ujumla, utukiaji wa mikakati kama hii ya kipragmatiki katika diskosi haswa ikiwa ya kiwango cha juu kama ilivyodhihirika katika mbinu ya umaanisho (50.74%), hufanya kufasirika kwa diskosi kama hizo na msomaji kuwa kugumu.

### 4.3.0 Fasiri ya Umma

Katika sehemu hii, tulijadili mikakati ya kipragmatiki inayotumiwa na umma kufasiri maana katika diskosi ya uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo*. Kwa kutumia mbinu ya hojaji, jumla ya watu wazima 50 walitoa majibu yao kulingana na maswali ambayo walikuwa wameulizwa katika hojaji. Katika hojaji husika, maswali yaligawanywa katika sehemu tatu; sehemu ya A ilijumuisha maswali yanayodhamiria kupima fasiri za diskosi kwa kuzingatia mbinu ya umaanisho, sehemu ya B nayo ilipima fasiri za diskosi kwa kutumia mbinu ya kinaya. Hatimaye sehemu ya C ilinuia kupima uwezo wa msomaji kufasri makala kwa kutumia mbinu ya jazanda. Mbinu hizi tatu zilizotukia kwa wingi katika nakala za gazeti la *Taifa Leo* ni miongoni mwa mbinu nyingi za kipragmatiki zinazozua utata katika kufasiri habari. Ili kumfanya mhojiwa asichoshwe na maswali mengi, tuliamua kuzitumia mbinu hizo tatu katika kuandaa hojaji yetu. Tazama muhtasari wa fasiri za umma katika jedwali 2 hapo chini.

**Jedwali 2: Ufasiri wa Umma kwa Kuzingatia Mikakati ya Kipragmatiki**

| Mikakati ya Kipragmatiki | Majibu Sahihi 0-2 | Asilimia (%) | Majibu Sahihi 3-5 | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Umaanisho | 17 | 34 | 33 | 66 |
| Kinaya | 32 | 64 | 18 | 36 |
| Jazanda | 21 | 42 | 29 | 58 |

### 4.3.1 Fasiri kwa Kuzingatia Mbinu ya Umaanisho

Jumla ya wahojiwa 50 walishiriki katika kujibu maswali matano yaliyoulizwa katika hojaji iliyotolewa. Kati ya washiriki 50, jumla ya wahusika 17 waliweza kupata kati ya sufuri na mbili (0-2) kwa tano ya majibu sahihi. Hii iliwakilisha asilimia thelathini na nne (34%) ya wahojiwa wote. Washiriki thelathini na tatu (33) walipata kati ya tatu na tano (3-5) kwa tano ya majibu sahihi. Hii iliwakilisha asilimia sitini na sita (66%) ya wahojiwa wote. (Rej. Jedwali 2 uk. 52). Baadhi ya majibu yaliyotolewa na washiriki ni kama yafuatayo:

Swali la kwanza liliuliza hivi;

*Bw. Ntimama alisema watu wengi wameendelea kuingia humo (msituni) siku za hivi majuzi kwa matumaini ya kulipwa fidia ambayo serikali imeahidi watakaohamishwa (Taifa Leo, 29/7/2009, uk. 2).* Je, unafikiri kuwalipa maskwota fidia ni njia mwafaka ya kuwaondoa watu misituni?

(A) Ndio [ ]

(B) La [ ]

(C) Sijui [ ]

Eleza jawabu lako kwa ufupi: ...........................................................................

Jawabu mwafaka lililotarajiwa kuchaguliwa ni (A). Maelezo ni kuwa hiki ni kishawishi cha kuwafanya maskwota waliovamia msitu huo kuweza kuondoka ili msitu uweze kuhifadhiwa na serikali na hili ndilo lengo la serikali.

Hata hivyo, takriban wahojiwa kumi na tano (15) ya washiriki wote hamsini (50) walichagua aidha jawabu la (B), au la (C). Mmoja wao (Rej. H12, uk. 94) akasema ya kuwa:

(16) *Kwa sababu wengi wasiokuwa hata maskwota watajitokeza.*

Mwingine aliyechagua jawabu lisilo sahihi alisema ya kuwa:

(17) *Wengine watazidi kuingia misituni kusudi walipwe fidia.* (Rej. H05, uk. 89)

Katika hojaji H03, uk.88, mshiriki alisema kwamba:

(18) *Misituni siyo makaazi yao ya kudumu. Wao ni maskwota.*

Mshiriki mwingine katika H02, uk. 87, alisema hivi:

(19) *Wakilipwa fidia maskwota hao wataendelea kuishi kama maskwota maana watafuja pesa hizo na huenda wasipate makao kwengine.*

Hawa wahojiwa wote na wengine ambao hawakuchagua jawabu la (A) walikosa kutambua mbinu ya umaanisho iliyodhamiriwa na serikali kwa kuamua kutoa fidia kwa watakaohiari kuhama kutoka msituni. Fasiri yao ya diskosi hiyo ni potovu kwani kwa muktadha wa suala la uhifadhi wa misitu, lengo kuu la serikali ni kuwashawishi waliouvamia msitu huo kuondoka kutoka katika msitu husika. Kwa mujibu wa Hofmann (1993), wakati wowote lugha inapotumiwa, huwa kuna mzungumzaji na dhamira yake. Aghalabu dhamira hii yake huwa imefichika katika maana iliyowazi ya yale anayosema. Kwa hivyo kwa msomaji asiyetambua mbinu ya umaanisho huenda akafasiri habari iliyoandikwa kwa njia isiyofaa.

Katika swali la tatu jumla ya wahojiwa kumi na tisa ya wahojiwa wote hamsini walitoa majibu yasio sahihi. Hii iliwakilisha asilimia thelathini na nane (38%) ya wahojiwa wote. Swali la tatu liliuliza hivi:

*Baadhi ya maskwota wamekuwa wakiishi katika maeneo ya msitu huo (Mau) kwa zaidi ya miaka hamsini (Taifa Leo,17/7/2008, uk.10).* Je, unadhani maskwota hao wana haki ya kuendelea kuishi katika msitu huo?

(A) Ndio [ ]

(B) La [ ]

(C) Sijui [ ]

Eleza jawabu lako kwa ufupi: ...........................................................................

Jawabu sahihi lilikuwa (B). Maelezo ni kuwa kwa kuendelea kuishi humo msituni hao maskwota watazidi kuuharibu msitu huo ilhali serikali imenuia kuuhifadhi.

Baadhi ya majibu yasiokuwa sahihi ambayo yalitolewa ni kama yafuatayo:

Mhojiwa katika H6 alichagua jawabu (A). Katika maelezo yake alisema ya kuwa:

(20) *Muda huu wote wamekaa katika msituni serikali ilikuwa wapi kuwaondoasha. Baadhi ya maskwota wana vyeti vya umilikaji ardhi kwa hivyo wana haki.*

Katika hojaji nambari H7, uk. 92, mhojiwa alichagua jawabu (A) na kutoa maelezo yafuatayo:

(21) *Msitu Mau umekuwa kama nyumbani kwa miaki mingi sana. Wana haki ya kuishi pale.*

Mifano tuliyotoa hapo juu inadhihirisha jinsi ambavyo ufasiri wa diskosi ya uhifadhi wa misitu kwa kupuuza mikakati ya kipragmatiki unavyosababisha juhudi za kuhifadhi misitu nchini Kenya kutatizika. Ama kwa hakika asilimia thelathini na nane (38%) ya wahojiwa ambao walitoa majibu yasiyo sahihi ni ya kiwango ambacho hakiwezi kupuuzwa.

Jawabu sahihi lililotarajiwa katika swali nambari 5 katika sehemu hiyo hiyo ya kwanza ya hojaji lilikuwa (B). Rejelea swali jinsi lilivyowasilishwa hapo chini:

*Wabunge hao walisema kuwa jamii kama zile za Ogiek zimezoea kuishi msituni na hazina mahali pengine pa kwenda (Taifa Leo, 30/11/2009, uk.7).* Unafikiri hali kama hii itaathiri juhudi za kuhifadhi msitu?

(A) La [ ]

(B) Ndio [ ]

(C) Sina habari [ ]

Eleza jawabu lako kwa ufupi: ..........................................................................

Kuendelea kuishi msituni kwa jamii kama vile Ogiek kutazidisha kuharibika kwa msitu huo kwani hao ni binadamu ambao wana shughuli mbalimbali za kujitafutia namna ya kujikimu kimaisha kama vile kutema kuni za kupikia, kuwinda, kujenga makao na kadhalika.

Mhojiwa nambari H43, uk.111, baada ya kuchagua jawabu la (A), alitoa maelezo yafuatayo:

(22) *Hii ni kwa sababu Ogiek hutumia tu misitu kama nyumbani kwao na wala hawaharibu misitu kwa kukata miti.*

Kwa upande mwingine, mhojiwa nambari H34, uk.107, aliyechagua jawabu la (A) alieleza ifuatavyo:

(23) *Kwa sababu ni mazoea ya kwamba kwa upande wa wabunge wanafikiri hizi jamii zimezoea kuishi msituni lakini kwangu binafsi naona ni njia ya kunyima jamii hizi ardhi na kuelezwa jinsi ya kukubali kuishi kama watu wengine.*

Maelezo ya wahojiwa hao wawili yanadhihirisha jinsi ambavyo hawazingatii suala zima la uhifadhi wa misitu bali kuunga mkono kuendelea kuishi msituni kwa jamii zinazoishi msituni. Wawili hao na wengine ambao walikosa kuchagua jawabu la (B) hawakuzingatia umaanisho unaojitokeza katika usemi wa wabunge katika dondoo la hapo juu na ndio sababu wakatoa fasiri kama hiyo waliyotoa. Jamii za Ogiek zikiendelea kuishi msituni bila shaka zitauharibu msitu huo kwa njia moja au nyingine. Hali kama hii itaathiri juhudi za serikali za kuhifadhi misitu nchini Kenya.

Kwa ujumla wahojiwa kumi na saba (17) kwa hamsini (50) walikosa kuchagua jawabu sahihi. Idadi hii iliwakilisha asilimia thelathini na nne (34%) ya wahojiwa wote. Hii ni asilimia ambayo itakuwa na athari hasi kwa shughuli za kuhifadhi misitu.

### 4.3.2 Fasiri kwa Kuzingatia Mbinu ya Kinaya

Katika sehemu ya B ya hojaji iliyotumiwa kupata data ya kufanikisha utafiti huu wetu kulikuwa na maswali ambayo yalinuia kupima uwezo wa mhojiwa kufasiri diskosi ya uhifadhi wa misitu nchini Kenya kwa kuzingatia mkakati wa kipragmatiki wa kinaya. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali tano (5). Jumla ya wahojiwa thelathini na mbili (32) kwa hamsini (50) walipata kati ya sufuri (0) na mbili (2) kwa alama zote tano (5) zilizotengewa sehemu hiyo. Hali hii ilichukuliwa kuwa ya chini ya wastani. Idadi hii iliwakilisha asilimia sitini na nne (64%) ya wahojiwa wote. Wahojiwa waliosalia walipata

kati ya tatu (3) na (5) kwa jumla ya alama zote tano. Hii ilikuwa asilimia thelathini na sita (36%) ya wahojiwa wote na ambayo ilichukuliwa kuwa juu ya wastani. Baadhi ya maswali na majibu yaliyotolewa na wahojiwa na ambayo hayakuwa sahihi ni kama yafuatayo: (Rej. Swali la 1 uk. 106)

*Wabunge kumi kutoka mkoa wa Rift Valley walikerwa mno jana na hatua ya serikali ya kuwataka maskwota katika msitu wa Mau waondoke humo ifikapo Oktoba (Taifa Leo, 17/7/2008, uk.10).* Unafikiri wabunge hao wana nia ya kuhifadhi msitu wa Mau?

(A) La [ ]

(B) Ndio [ ]

(C) Sijui [ ]

Eleza jawabu lako kwa ufupi: .............................................................

Jawabu sahihi lililotarajiwa katika swali hili lilikuwa (B). Wabunge kama viongozi wa wananchi wanatarajiwa kuunga mkono hatua ya serikali ya kuhifadhi misitu nchini Kenya. Ni kinaya kuona wakipinga shughuli za kuhifadhi msitu. Hali hii ya wabunge hao kupinga shughuli za kuwahamisha maskwota ili kuhifadhi msitu wa Mau ni mbinu yao tu ya kisiasa ya kuonekana kuwaunga mkono maskwota hao ambao waliuvamia msitu huo.

Mhojiwa nambari thelathini na nne (H34), uk.106, alichagua jawabu la (A) na akatoa maelezo yafuatayo:

(24) *Kwangu naona ni njia ya ufisadi. Nia zao sio za kawaida ni za kiunyama.*

Mhusika huyu hajatambua kuwa kile wanachosema wabunge hao ni kinaya na kwamba suala la kuhifadhi msitu wa Mau ni la umuhimu mkubwa na linapaswa kuungwa mkono na watu wote wanaojali mazingira yao.

Katika hojaji H15, uk.97, mhojiwa alichagua jawabu (A) ambapo katika maelezo yake alisema ya kwamba:

(25) *Hiyo ndiyo silaha wanayotumia kupata kura kuwa hao ni watetezi wa wananchi.*

Kwa kuchagua jawabu alilochagua kisha akatoa maelezo aliyotoa ni ishara ya kuonyesha kwamba mhojiwa huyo hajafasiri habari ya wabunge hao vilivyo. Inafaa ieleweke kwamba wabunge kama viongozi katika jamii, wanaendeleza mipango mizuri ya serikali kama vile uhifadhi wa misitu nchini Kenya. Hali kama hii ya kufasiri habari na wasomaji kwa njia isiyofaa inatokana na matumizi ya mbinu ya kinaya ambapo mwandishi huwa amekiuka kauli ya kiasi. Kwa mujibu wa Bloomer (2005) kauli ya kiasi inamhitaji mwandishi kuyafanya maandishi yake kumfahamisha msomaji wake kadri iwezekanavyo. Kutoa habari isiyokamilika kisha kumwachia msomaji kufasiri habari hiyo kwa uchukulio kwamba ataelewa dhamira ya mwandishi husababisha hali kama hiyo hapo juu ambapo msomaji wa habari husika hutoa ufasiri ambao sio kamili.

Swali la tatu katika sehemu hii ya B katika hojaji iliyotumiwa kupata data kuhusu mbinu hii ya kinaya lilijibiwa visivyo na wahojiwa wapatao thelathini na sita (36) kati ya wahojiwa wote hamsini. Hii iliwakilisha asilimia sabini na mbili (72%) ya wahojiwa wote. Swali lenyewe liliuliza ifuatavyo:

*Punde tu baada ya kuchapishwa kwa notisi hiyo (kuondoka msituni), waziri mkuu Raila Odinga ambaye anasimamia wizara zote alipinga hatua hiyo na kuwaagiza wakaazi wasiondoke hadi suluhisho kamili lipatikane (Taifa Leo, 28/8/2009, uk. 1).*

Je, unakubaliana na msimamo wa Waziri Mkuu?

(A) La [ ]

(B) Ndio [ ]

(C) Sijui [ ]

Eleza jawabu lako kwa ufupi: ...........................................................................

Tulitarajia wahojiwa kuchagua jawabu la (A). Ni kinaya kumsikia waziri mkuu akipinga shughuli za kuwahamisha maskwota kutoka katika msitu wa Mau ilhali yeye ndiye aliongoza shughuli nzima ya kuwafurusha waliouvamia msitu huo. Waziri mkuu kama kiongozi wa serikali bila shaka alihusika katika uamuzi wa kutoa ilani ya kuwataka maskwota kuuhama msitu huo wa Mau. Kulingana na usemi wake waziri mkuu, kuna sababu fulani fiche inayomfanya kutoa usemi kama huo. Kwa hivyo, kile ambacho Waziri mkuu anasema si kile anadhamiria. Hali kama hii ya kuacha habari muhimu kwa msomaji wako ndio humfanya msomaji kufasiri habari kwa njia potofu.

Baadhi ya maelezo yaliyotolewa na wahojiwa ni kama ifuatavyo:

(26) *Waziri mkuu yuko na tarajio la mpangilio fulani ambao angependa utumiwe ili kuwatoa maskwota hawa msituni*. (Rej. H40, uk.110).

Maelezo haya yanadhihirisha jinsi ambavyo msomaji katika ufasiri wake alipuuza mbinu ya kinaya ambayo inajitokeza katika usemi wa Waziri mkuu katika swali lililoko hapo juu.

Mhojiwa nambari H35 aliyechagua jawabu (A), naye anaeleza jawabu lake ifuatavyo:

(27) *Wangeondoka kwenda wapi*?

Mhusika huyu hajatambua kuwa usemi wake Waziri mkuu unadhihirisha kinaya na kwa hivyo ufasiri wake ni sharti utilie maanani hali hiyo. Kwa mujibu wa Leech (1983), kanuni ya kinaya hufanya kazi pamoja na kanuni za ushirikiano na upole katika mawasiliano. Hata hivyo, kanuni ya kinaya humwezesha mzungumzaji au mwandishi kutokuwa mpole huku akionekana kuwa mpole. Katika kufanya hivyo, mwandishi huwa amedumisha ushirikiano wa kijamii akiwa na lengo la kufanikisha mawasiliano.

### 4.3.3 Ufasiri wa Kijazanda

Sehemu ya C ya hojaji iliyotumiwa kama chombo cha kukusanya data ilihusisha jumla ya maswali matano ambayo yalidhamiria kupima uwezo wa mhojiwa kufasiri habari ya uhifadhi wa misitu kwa misingi ya mbinu ya jazanda.

Jumla ya wahojiwa hamsini walijibu maswali yaliyoulizwa katika sehemu hii. Wahojiwa 21 walipata alama kati ya 0 na 2 kwa jumla ya alama tano ya majibu sahihi. Wahojiwa hao waliwakilisha asilimia arobaini na mbili (42%) ya wahojiwa wote hamsini. Kiwango hiki kilichukuliwa kuwa cha chini ya wastani. Jumla ya wahojiwa ishirini na tisa (29) walipata alama kati ya 3 na 5 kwa jumla ya alama tano za majibu sahihi. Hii iliwakilisha asilimia hamsini na nane (58%) ya wahojiwa wote. Kiwango hiki kilichukuliwa kuwa cha juu ya wastani. (Rej. jedwali 2 uk. 52).

Ifuatayo ni mifano ya maswali yaliyoulizwa na majibu ambayo yalitolewa na wahojiwa mbalimbali. Swali la kwanza katika hojaji iliyotumika kusanya data liliuliza hivi:

> *Tena si kupanda miti kwa ajili ya kuvutia mvua pekee. Wakulima hao wamegundua dhahabu inayopatikana katika miti aina hizo mbili (Taifa Leo, 29/5/2009, uk.21).*

Je, unakubaliana na hoja kuwa dhahabu inapatikana katika miti? Eleza kwa ufupi.

Tulitarajia wahojiwa kuunga mkono kauli ya usemi kwa sababu miti ina manufaa mengi na hutuletea utajiri mkubwa sawa na dhahabu. Neno *dhahabu* limetumika kijazanda katika usemi huo kwa hivyo fasiri iliyo sawa itategemea ufahamu wa mfasiri kuwa kuna matumizi ya jazanda na ni muhimu atambue maana ya jazanda hiyo. Mhojiwa mmoja alitoa jibu lifuatalo:

(28) *La, huo ni usemi tu kwa sababu haijadhibitishwa kisayansi kama dhahabu inaweza kupatikana kwa miti.* (Rej. H12, uk.94).

Mhojiwa mwingine, (Rej. H29, uk.105), alitoa maelezo yafuatayo:

(29) *Sina ukweli wa kuridhisha lakini sikubaliani na hoja kuwa dhahabu hupatikana katika miti. Dhahabu mara kwa mara hupatikana mahali pagumu kama kwenye mawe na miamba.*

Fasiri kama hii inadhihirisha jinsi wasomaji wengi wa diskosi ya uhifadhi wa misitu hushindwa kutoa fasiri mwafaka ambayo itawawezesha kuelewa ujumbe uliodhamiriwa na mwandishi wa habari kama hiyo. Matumizi ya jazanda katika usemi huficha ujumbe wa usemi husika ambapo msomaji huhitajika kuufichua ndipo aweze kuelewa maana

iliyodhamiriwa na mwandishi. Hali hii ya kuficha ujumbe fulani wa usemi hukiuka kanuni ya jinsi ambayo kwa mujibu wa Grundy (2000) humhitaji mwandishi kutofumba mazungumzo yake na kutozua utata katika maandishi yake.

Swali la nne katika sehemu ya C lilikuwa ifuatavyo:

*Suala hilo (Msitu wa Mau) sasa limegeuka kama mpira unaorushwa huku na kule kati ya Rais, Waziri Mkuu na wabunge wa mkoa wa Bonde la Ufa. Tutaendelea kupiga mpira mpaka lini. (Taifa Leo, 4/9/2009, uk. 5).* Fafanua sehemu iliyopigiwa mstari kwa kifupi.

Katika kulijibu swali lililoulizwa hapo juu, mhojiwa mmoja, (Rej. H13, uk. 95) alitoa maelezo yafuatayo:

(30) *Wahusika hawana nia moja katika matamshi yao.*

Naye mhojiwa katika H29, uk. 105 alieleza jibu lake ifuatavyo:

(31) *Suala la msitu wa Mau linarushwarushwa kama mpira kwa kuwa wabunge na viongozi wengi wanahusika kwa hivyo wanapeana rushwa mmoja kwa mwingine halafu wamekuwa wafungwa na mateka wa utamu wa pesa kuliko uhai wa misitu.*

Wahojiwa hao wawili hawakuelewa jazanda iliyotumika katika usemi wa hapo juu hivyo basi waliufasiri visivyo ujumbe uliodhamiriwa na mwandishi wa habari hiyo. Tulitarajia wahusika kuelewa kuwa jazanda hiyo ilikuwa na maana kuwa suala hilo la msitu wa Mau litandelea kutafutiwa suluhu kwa muda usiojulikana. Utafutaji wa suluhu la msitu wa Mau umekuwa kama mpira ambao unarushwa huku na huko. Hali hiyo ya wasomaji hao wawili kutofasiri habari vilivyo ilitokana na mwandishi kutompa msomaji maelezo ya kutosha kumwezesha kuelewa dhamira yake. Mwandishi alikiuka kanuni za kiasi na jinsi kama zilivyojadiliwa katika sura ya kwanza. Mhojiwa 29 anachukulia kwamba wahusika katika msitu wa Mau wanashiriki kutoa rushwa fasiri ambayo inamfanya kupotoka kabisa na hivyo basi kupata ujumbe ambao haukudhamiriwa na mwandishi wa makala hiyo.

Katika swali la 5 katika sehemu ya C ya hojaji (Kiambatisho1 uk.85), wahojiwa 16 walitoa majibu yasiyo sahihi. Swali hilo liliuliza ifuatavyo:

*'Kama serikali naamini tunaweza kutafuta mbinu za kustawisha msitu huo' akaeleza Bw. Odinga (Taifa Leo, 16/7/2008, uk.4).* Katika muktadha huu, serikali ni nani? Eleza kwa ufupi.

Jawabu ambalo lilitarajiwa ni kuwa, Bw. Odinga amehusisha kila mmoja ambaye yuko katika serikali. Anaposema *...naamini tunaweza...* amejumuisha wale wote ambao wanahusika katika juhudi za kulitafutia suala hilo la msitu wa Mau suluhisho kamili. Bw. Odinga hakutaka hali ambapo yeye binafsi anachukuliwa kama anayeongoza katika kulitafutia suluhisho suala la msitu wa Mau.

Fasiri mbalimbali zilitolewa na wahojiwa ambapo upotovu katika kufasiri dondoo hilo ulidhihirika. Mhojiwa nambari H01, uk. 88, alijieleza ifuatavyo:

(32) *Waziri Mkuu ndiyo serikali na Rais Kibaki.*

Kwa upande mwingine, mhojiwa nambari H22, uk. 102, alijieleza ifuatavyo:

(33) *Waziri Mkuu, kwa sababu anawakilisha serikali wakati anapozungumza.*

Mhojiwa huyu alichukulia serikali kumaanisha Waziri Mkuu.

Mhojiwa H16, uk. 98, naye alijieleza ifuatavyo:

( 34) *Serikali hapa ni Bw. Odinga kwa vile anaelewa kwamba mwanasiasa ambaye ataendesha suala hili vizuri, maskwota hawa watampenda na watampa kura mwaka 2012.*

Maelezo hayo ya hao wahojiwa yanadhihirisha kupuuza kwao kwa mkakati wa kipragmatiki ambao ungewasaidia katika kufasiri habari husika. Kiambishi {*–tu*} katika kitenzi *tunaweza* ni kiwakilishi cha nafsi ya kwanza katika wingi. Hali kama hii inawajumuisha wote ambao wamo serikalini. Uamuzi unaotolewa kuhusu suala la uhifadhi wa msitu wa Mau kwa hivyo, ni wa kundi nzima wala sio wa mtu mmoja. Waziri Mkuu alikiuka kanuni ya kiasi katika matumizi yake ya kiwakilishi hicho cha nafsi kwani amemnyima msomaji wa usemi wake

habari zaidi ambayo ingemsaidia katika kufanikisha kufasiri usemi huo vilivyo. Kanuni ya kiasi kwa mujibu wa Leech (1983) inasema ya kwamba mwandishi anapaswa kumfahamisha msomaji wake kadri iwezekanavyo.

### 4.3.4 Muhtasari

Katika sehemu hii, muhtasari wa fasiri za diskosi ya uhifadhi wa misitu kwa kuzingatia mikakati ya kipragmatiki ya umaanisho, kinaya na jazanda ulitolewa. Muhtasari huo ulinuia kumwezesha msomaji wa tasnifu hii kuelewa kwa urahisi yaliyotokana na fasiri kwa kuzingatia mikakati ya kipragmatiki iliyotajwa. Kati ya wahojiwa wote hamsini walioshiriki katika mahojiano hayo, asilimia thelathini na nne ya wahojiwa wote walitoa fasiri zilizokuwa potovu. Fasiri hizo zilipewa alama ya ubora ya kiwango cha chini cha kati ya sufuri na mbili (0-2) kwa tano katika mbinu ya umaanisho. Asilimia iliyosalia ya sitini na sita (66%) walitoa fasiri iliyopewa alama ya ubora ya juu ya wastani.

Katika kufasiri kwa kuzingatia mbinu ya kinaya, wahojiwa thelathini na wawili kati ya wahojiwa wote hamsini walidhihirisha fasiri zilizopewa alama ya ubora ya chini ya wastani. Hii iliwakilisha asilimia sitini na nne ya wahojiwa wote hamsini. Kiwango cha asilimia thelathini na sita (36%) cha wahojiwa wote hamsini walidhihirisha fasiri zilizopewa alama ya ubora ya kiwango cha juu ya wastani.

Wahojiwa ishirini na mmoja kwa wahojiwa wote hamsini walitoa fasiri iliyo chini ya wastani katika kuzingatia mkakati wa jazanda. Hii iliwakilisha asilimia arobaini na mbili (42%) ya wahojiwa wote. Asilimia iliyosalia ya hamsini na nane (58%) ya wahojiwa wote iliwakilisha wahojiwa ambao walitoa fasiri iliyokuwa juu ya wastani. Katika mikakati yote mitatu ya kipragmatiki yaani umaanisho, kinaya na jazanda ambayo ilirejelewa katika fasiri ya diskosi ya uhifadhi wa misitu ni mbinu ya kinaya ambayo ilidhihirisha kutatiza ufasiri wa wasomaji kwa kiwango kikubwa (64%). Mbinu hii ilifuatiwa na mbinu ya jazanda (42%) na mwisho, umaanisho (34%). Asilimia hizi ni za kiwango ambacho hakiwezi kupuuzwa haswa tunapochukulia kuwa diskosi za uhifadhi wa misitu hudhamiria kuchochea wanaozisoma kushiriki katika shughuli za kuhifadhi misitu. Iwapo wasomaji wengi kiasi kama hicho kilichowakilishwa na asilimia zilizorejelewa hapo juu wataweza kufasiri habari visivyo basi

juhudi za serikali za kuhimiza shughuli za kuhifadhi misitu zitakosa kufaulu jinsi ilivyotarajiwa. Uchanganuzi huu wa kitakwimu umewasilishwa kwa muhtasari katika jedwali nambari 2, ukurasa 52.

### 4.4.0 Athari ya Ufasiri wa Kipragmatiki

Mojawapo ya malengo ya utafiti huu ilikuwa kueleza athari ya ufasiri wa kipragmatiki wa habari ya uhifadhi wa misitu kwa shughuli za uhifadhi wa misitu. Fasiri mbalimbali zilizotolewa na wahojiwa zilitathminiwa na kuhusishwa na shughuli za uhifadhi wa misitu. Wahojiwa ambao walifasiri habari juu ya uhifadhi wa misitu kwa kuonyesha kuwa hawakuwa tayari kuunga mkono shughuli nzima ya uhifadhi wa misitu walichukuliwa kuwa katika mstari wa mbele kudhoofisha juhudi za uhifadhi wa misitu. Kwa mujibu wa Leech (1983:32), nadharia ya Grice (1975) ya umaanishi wa kimaongezi ilibuniwa naye Grice (1975) ili kuweza kuyaeleza matamshi ambapo mzungumzaji au mwandishi huelekea kuwa na maana zaidi ya yale anayosema au kuandika. Baadhi ya mifano ya matamshi ya wahojiwa kuhusu suala la kuhifadhi misitu ni kama yafuatayo:

Katika hojaji (kiambatisho1) sehemu ya A, swali nambari moja liliuliza mhojiwa iwapo alifikiria kuwa kuwalipa maskwota fidia ilikuwa njia mwafaka ya kuwaondoa misituni. Mhojiwa nambari H21, uk.101, alitoa jawabu lifuatalo:

(35) *Watu wengi wataendelea kuingia msituni kwa nia ya kunufaika.*

Huyu ni mhusika ambaye anaziona juhudi za kuwahamisha maskwota kutoka katika msitu kwa kuwafidia kama nafasi ya kujinufaisha. Iwapo watu watakuwa na mtazamo kama huo basi misitu yetu itazidi kuvamiwa na kukosa kuhifadhiwa.

Naye mhojiwa nambari H23, uk. 103 ambaye alipinga kufidiwa kwa maskwota alisema hivi kuhusu swali hilo la kwanza:

(36) *Kwa sababu hawawezi kupata mashamba mengine kama yale wanaofukuzwa ndani.*

Iwapo tutachukulia kwamba hao maskwota hawawezi kupata mashamba kwingineko hivyo basi waendelee kuishi misituni, misitu itaendelea kuharibiwa na hao maskwota. Lengo kuu

ambalo lapaswa kushughulikiwa na kila mtu ni kuhakikisha ya kwamba misitu imehifadhiwa. Lengo hilo halitaafikiwa iwapo tutaanza kuwaruhusu maskwota kuendelea kuishi misituni kwa kisingizio kuwa hawawezi kupata mashamba mahali kwingineko. Mawazo kama haya ya kuwaonea maskwota huruma yalidhihirishwa na mhojiwa nambari H36, uk. 108 ambaye vile vile alipinga kuwapa maskwota hao fidia. Kauli yake ilikuwa ifuatavyo:

(37) *Wengi wao ni maskini na hawawezi kufuatilia taratibu za kununua shamba lingine.*

Kile ambacho mhusika huyu anaelekea kusema ni kwamba hao maskwota wasihamishwe kutoka msitu huo bali waendelee kuishi humo msituni. Hali ya kuendelea kuishi msituni ndiyo itafanya uhifadhi wa msitu husika kutatizika.

Mhojiwa nambari H07, uk. 91, ameathirika na imani ya utamaduni hivyo basi anapinga kufidiwa kwa maskwota hao kwa kuhoji ifuatavyo:

(38) *Kwa sababu wanadai eti walizaliwa huko na baba zao kazikwa kule msituni.*

Mhusika huyu anaelekea kuwaunga mkono hao maskwota kwa hilo dai lao. Anaamini kuwa kuondolewa mahali ulikozaliwa na babu zako kuzikwa si jambo la busara. Hata hivyo, hiyo si sababu tosha ya kuwaruhusu hao maskwota kuendelea kuishi msituni ilhali msitu huo umekabiliwa na hatari ya kuangamia na kusababisha hatari kubwa kwa kizazi cha sasa na hata kijacho.

Katika sehemu iyo hiyo ya A, swali nambari nne liliuliza mhojiwa ifuatavyo:

> *Tunaweza kupanda miti katika mashamba na kubakisha sehemu ndogo tu ya kupanda chakula (Taifa Leo, 28/8/2009, uk. 4).* Unafikiri maskwota hao wanamaanisha nini?
>
> (A) Wanahitaji chakula [ ]
>
> (B) Hawako tayari kuondoka kutoka msituni [ ]
>
> (C) Wanataka kupanda miti [ ]

Tulitarajia wahojiwa kuchagua jawabu la (B) kama lililosahihi kwa muktadha wa kauli ya maskwota hao. Hata hivyo, baadhi ya wahojiwa walichagua jawabu la (A), kwa mfano mhojiwa nambari H03, uk.88, H20, uk.100 na H21, uk.101. Kuwaruhusu maskwota hao kuishi msituni kwa kujishughulisha na kilimo kutazidisha tu uharibifu wa misitu kwani ili kupata sehemu ya kulima na kupanda mazao yao, maskwota hao wataikata miti katika msitu husika.

Swali la kwanza katika sehemu ya C ya hojaji iliyotumiwa kupata data katika utafiti huu liliuliza ifuatavyo:

> *Tena si kupanda miti kwa ajili ya kuvutia mvua pekee. Wakulima hao wamegundua dhahabu inayopatikana katika miti aina hizo mbili (Taifa Leo, 29/5/2009, uk.21).*

Je, unakubaliana na hoja kuwa dhahabu inapatikana katika miti? Eleza kwa ufupi.

Wahojiwa wengi walikubaliana na kauli hiyo kwamba dhahabu inapatikana katika miti. Wahojiwa hao waliweza kutambua kwamba dhahabu katika miti ni sawa na faida nyingi ambazo hupatikana katika bidhaa zinazotokana na miti. Ufasiri kama huu utawafanya wananchi kuona faida ya kuhifadhi misitu kwani faida za shughuli kama hiyo ni dhahiri kwao. Hata hivyo baadhi ya wahojiwa (17) walipinga kauli hiyo wakidai ya kwamba dhahabu hupatikana tu ardhini! Kwa mfano, mhojiwa nambari 24 alisema hivi:

(39) *Dhahabu haipatikani kwenye miti kuliko na udongo wa maji bali kwenye mawe mawe milimani.*

Fasiri ya aina hii ambayo ilitolewa na mhojiwa husika inadhihirisha kuwa jazanda (*dhahabu*) iliyotumiwa katika usemi huo ilizua utata ambao ulisababisha fasiri zisizo sahihi. Wahusika ambao watafasiri habari kuhusu uhifadhi wa misitu kwa namna hii bila shaka watapuuza umuhimu unaohusishwa na misitu. Hali kama hii itawafanya wahusika kukosa kutekeleza shughuli za kuhifadhi misitu kwani hawataona umuhimu wake.

Mhojiwa nambari H37, uk. 109, naye alipinga kauli hiyo kwa kusema hivi:

(40) *Hapana, kwa sababu madini huchimbwa na hayapatikani kwenye miti. Bila shaka hii ni porojo.*

Dhahabu ni kitu kilicho na dhamana kubwa. Kila mja hujishughulisha na kutumai kupata dhahabu wakati fulani maishani mwake. Fasiri iliyotolewa na wahusika hao wawili ni ishara ya kwamba hawawezi kujishughulisha na juhudi za kupata dhahabu ambayo hupatikana mitini kwani wanaona hii kama porojo tu.

Mhojiwa nambari H14, uk. 96, alitoa maelezo yafuatayo:

(41) *Sina ukweli kwa sababu wakati walikuwa wanaishi kwa usalama jambo hili la dhahabu halikujulikana.*

Mhusika huyu hakung'amua hata chembe maana ya jazanda iliyotumiwa katika usemi ambao ulidondolewa hapo juu. Kukosa kutambua maana ya jazanda husika katika usemi wa uhifadhi wa misitu kutawafanya wahusika kupuuza shughuli za uhifadhi wa misitu kama vile kupanda miti zaidi kwa vile hawataona umuhimu wake. Matumizi ya jazanda kama ilivyodhihirika hapo juu hukiuka kanuni ya jinsi kwa mujibu wa Grundy (2000) anayesema kuwa mwandishi au mzungumzaji hastahili kufumba mazungumzo yake. Hali hii huzua utata katika kufasiri habari husika ambapo mfasiri hujitokeza na ufasiri ambao si sawa hivyo basi kupotosha ujumbe uliodhamiriwa na mwandishi. Kwa mujibu wa Ochwal (2008), lengo la namna yoyote ya mawasiliano ni kupitisha ujumbe ili ujumbe huo unapowasilishwa kwa mpokeaji uweze kufasiriwa vilivyo. Iwapo upitishaji wa habari utakuwa na dosari yoyote, basi ufasiri wake utapotosha ujumbe hivyo basi kukosa kuafikia madhumuni ya mawasiliano. Jinsi tulivyoona hapo juu, matumizi ya jazanda huchangia kutatiza kupitishwa kwa habari kwa njia iliyoshwari. Hali hii hatimaye hutatiza mawasiliano baina ya wahusika.

### 4.4.1 Hitimisho

Mifano ambayo imetolewa hapo juu inadhihirisha jinsi ambavyo ufasiri wa diskosi ya uhifadhi wa misitu kwa kutozingatia mikakati ya kipragmatiki unavyoweza kuwa na athari mbalimbali jinsi ilivyodhihirishwa. Wahusika ambao watakuwa na ufahamu wa mbinu za kipragmatiki ambazo zitakuwa zimetumika katika diskosi husika wataweza kuifasiri vilivyo huku wale wahusika ambao hawatakuwa na ufahamu wa mikakati ya kipragmatiki ambayo

itakuwa imetumika watajitokeza na fasiri ambazo zitapotosha ujumbe ambao utakuwa umedhamiriwa na mwandishi wa makala husika.

Kwa mujibu wa Toili (2000), ili wakazi wa mashinani wanufaike na shughuli za kuhifadhi mazingira, mwito wa kimazingira lazima ulenge katika kuwasilisha masuala yote kwa wanaolengwa pamoja na kuweka wazi matokeo na mapendekezo yanayotokana na shughuli hizo. Kwa kufanya hivyo, kanuni za mawasiliano, ushirika na usawa huimarisha usimamizi wa mazingira. Utafiti huu umeweza kubaini kuwa ufasiri usiofaa wa habari kuhusu misitu hutokana na wahusika kushindwa kung'amua maana ya mikakati mbalimbali ya kipragmatiki ambayo huwa imetumiwa katika makala husika. Athari inayotokana na hali kama hii ni kuwa wahusika hukosa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kuhifadhi misitu kama vile kutokata miti kiholela, kupanda miti mingine na hata kutojenga makao misituni.

Katika utafiti huu, matumizi ya mbinu ya kinaya yamedhihirika kusababisha utata wa ufasiri wa makala husika kwa asilimia sitini na nne (64%) ya majibu sahihi yaliyokuwa chini ya wastani yaani kati ya sufuri (0) na mbili (2). Mbinu hii ilifuatiwa na jazanda ambayo ilidhihirisha asilimia arobaini na mbili (42%) ya majibu sahihi yaliyokuwa chini ya wastani. Kwa hivyo, matumizi ya mikakati sampuli hii ya kipragmatiki katika diskosi yoyote ile ya uhifadhi wa misitu kama ilivyodhihirika katika nakala za gazeti la *Taifa Leo* zilizotumiwa katika utafiti huu (Rej. Kiambatisho 2 uk. 112), yatazua utata katika kufasiri makala husika. Hali kama hii huenda ikatatiza mawasiliano kati ya mwandishi na msomaji wake na kupelekea juhudi za kuhifadhi misitu kukwama.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa utafiti wetu. Aidha taamuli kwa misingi ya maswali, malengo na nadharia ya utafiti huu inatolewa. Mjadala kuhusu iwapo matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha malengo ya utafiti wenyewe umefanywa. Aidha, mapendekezo yametolewa kwa mujibu wa utafiti uliofanywa ili kuwapa watafiti wengine hamu ya kuendeleza tafiti zinazohusu uhifadhi wa misitu kwa njia ya kimawasiliano.

## 5.2 Muhtasari

Madhumuni ya utafiti huu ilikuwa kuchanganua ufasiri kipragmatiki wa diskosi ya uhifadhi wa misitu nchini Kenya. Katika kuafikia madhumuni hayo, maswali yafuatayo mahsusi yalitusaidia: Je, kuna mikakati yoyote ya kipragmatiki inayotumiwa katika diskosi ya uhifadhi wa misitu ili kuwasilisha ujumbe na maana zilizokusudiwa? Umma unatumia njia zipii ili kufasiri maana katika habari juu ya uhifadhi wa misitu? Kuna athari zipi za ufasiri kipragmatiki wa habari juu ya uhifadhi wa misitu katika shughuli za kuhifadhi misitu? Haya ndiyo maswali tuliyoshughulikia katika sura ya nne.

Ili kupata majibu ya maswali hayo hapo juu, uchanganuzi wa yaliyomo katika nakala zote thelathini na sita (36) za gazeti la *Taifa Leo* za baina ya mwaka wa 2008 na 2009 ulifanywa ili kubaini kuwepo kwa mikakati ya kipragmatiki. Data iliyokusanywa kutokana na uchanganuzi huo ilidhihirisha kuwa kuna matumizi ya mikakati ya kipragmatiki katika diskosi za uhifadhi wa misitu. Jumla ya mikakati aina sita ilidhihirika katika nakala hizo thelathini na sita za gazeti la *Taifa Leo* zilizotumiwa katika utafiti huu. Kati ya mikakati hiyo yote, mbinu ya umaanisho ilitukia mara nyingi ya zote (34) ikifuatiwa na kinaya (17), methali/semi (07) kisha jazanda (06). Matumizi ya vivumishi na uongo yalitukia mara chache sana-mara mbili na moja mtawalia. Hali hii ilidhihirisha kwamba katika diskosi za uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo* kuna utata wa

kiwango fulani ambao unahitaji kufafanuliwa ili ujumbe ambao umehimiliwa katika makala husika uweze kueleweka wazi wazi kwa msomaji.

Aidha uchanganuzi wa data iliyotokana na hojaji iliyojazwa na wahojiwa ulionyesha kwamba fasiri zisizosahihi za diskosi za uhifadhi wa misitu zilizohusishwa ziliongozwa na mbinu ya kinaya ambayo ilikuwa asilimia sitini na nne (64%) ya wahojiwa wote. Katika nafasi ya pili kulikuwa na jazanda kwa asilimia arobaine na mbili (42%) na mwisho mbinu ya umaanisho iliwakilisha asilimia thelathini na nne (34%). Kutokana na hali hii (Rej. Jedwali 2 uk. 52), tunaweza tukasema ya kwamba matumizi ya mbinu ya kinaya katika diskosi ya uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo* huenda ikazua utata mkubwa utakaomtatiza msomaji wa diskosi husika kiasi cha kwamba fasiri ya habari hiyo huenda ikatatizika na hivyo basi kupotosha ujumbe uliodhamiriwa na mwandishi. Hali ikiwa hivi, shughuli za uhifadhi wa misitu hazitatekelezeka jinsi ilivyotarajiwa.

Hatimaye, uchanganuzi wa athari zinazotokana na uzingatiaji wa mikakati ya kipragmatiki katika kufasiri diskosi ya uhifadhi wa misitu ulifanywa ambapo ilijitokeza wazi wazi kuwa wahusika ambao walishindwa kung'amua maana ya baadhi ya mikakati ya kipragmatiki iliyokuwa imetumika katika diskosi husika, walishindwa vile vile kutoa fasiri kamili za diskosi hizo za uhifadhi wa misitu. Hali hii ilikuwa kinyume na wahusika ambao walitambua maana ya mikakati ya kipragmatiki iliyokuwa imetumika katika diskosi husika kwani waliweza kutoa fasiri iliyokuwa mwafaka.

## 5.3 Taamuli

Madhumuni ya utafiti huu ilikuwa kuchanganua ufasiri kipragmatiki wa diskosi ya uhifadhi wa misitu nchini Kenya. Ili kuafikia madhumuni hayo, utafiti huu ulijikita katika malengo mahsusi yafuatayo: kubaini mikakati ya kipragmatiki inayotumiwa katika diskosi juu ya uhifadhi wa misitu ili kupitisha ujumbe ulionuiwa, kujadili njia mbalimbali zinazotumiwa na umma kufasiri maana katika habari juu ya uhifadhi wa misitu na mwisho, kueleza athari zinazotokana na ufasiri wa kipragmatiki wa habari za uhifadhi wa misitu kwa shughuli za kuhifadhi misitu.



MASENO UNIVERSITY
S.G. S. LIBRARY

### 5.3.1 Mikakati ya kipragmatiki

Kwa mujibu wa utafiti huu, jumla ya mikakati sita (6) ya kipragmatiki ilibainishwa katika diskosi ya uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa Leo*. Hali hii iliafiki lengo la kwanza la utafiti huu. Utukiaji wa mikakati hiyo katika diskosi husika iliongozwa kwa idadi na umaanisho- asilimia hamsini nukta saba nne (50.74%), kinaya- asilimia ishirini na tano nukta tatu saba (25.37%), methali/semi asilimia kumi nukta nne nne (10.44%), jazanda- asilimia nane nukta tisa tano (8.95%), vivumishi- asilimia mbili nukta tisa nane (2.98%) na mwisho, uongo- asilimia moja nukta nne tisa (1.49%). Hali kama hii ya utukiaji wa mikakati ya kipragmatiki kama hiyo iliyodhihirika hapo juu inaonyesha jinsi ambavyo diskosi kama hizo huenda zikawa na utata katika kufasirika kwake.

### 5.3.2 Njia za kufasiri maana

Katika kuafikia lengo la pili katika utafiti huu yaani kujadili njia mbalimbali zinazotumiwa na umma kufasiri maana katika habari juu ya uhifadhi wa misitu, utafiti huu ulibaini kuwa mbinu za umaanisho, jazanda na kinaya zilitumiwa na umma kufasiri maana katika makala juu ya uhifadhi wa misitu nchini Kenya. Kwa kurejelea mbinu ya umaanisho, kati ya wahojiwa wote hamsini, asilimia sitini na sita (66%) walitoa fasiri iliyokuwa juu ya wastani ilhali asilimia thelathini na nne (34%) walitoa fasiri ambayo ilikuwa chini ya wastani. Katika kutumia mbinu ya kinaya ili kutoa fasiri, kati ya wahojiwa wote waliohojiwa, asilimia thelathini na sita (36%) walitoa fasiri iliyokuwa juu ya wastani ilhali asilimia sitini na nne (64%) walitoa fasiri ambayo ilikuwa chini ya wastani. Aidha katika matumizi ya mbinu ya jazanda na wahojiwa katika kufasiri maana, asilimia hamsini na nane (58%) ya wahojiwa wote walitoa fasiri zilizokuwa juu ya wastani huku asilimia arubaini na mbili (42%) wakatoa fasiri zilizokuwa chini ya wastani (Rej. Jedwali 2 uk. 52).

Kutokana na matokeo hayo wahojiwa wengi walitatizika kutoa fasiri ya maana iliyopatikana katika diskosi ya uhifadhi wa misitu haswa walipozingatia mbinu ya kinaya. Mbinu hii ilifuatiwa na jazanda kisha umaanisho.

### 5.3.3 Athari ya ufasiri kipragmatiki

Kutokana na utafiti huu, ufasiri wa makala kuhusu uhifadhi wa misitu kwa misingi ya pragmatiki una athari katika shughuli za kuhifadhi misitu. Lengo la tatu la utafiti huu liliafikiwa kwa kubainika kuwa wahojiwa ambao hawakuelewa kuwepo kwa mikakati ya kipragmatiki katika diskosi ya uhifadhi wa misitu walitoa fasiri ambazo zilikuwa za kiwango cha chini ya wastani kinyume na wenzao waliozingatia mikakati ya kipragmatiki. Kwa mfano data nambari 38 uk.66 inadhihirisha kuwa maskwota waliouvamia msitu wa Mau hawako tayari kuondoka. Hali ya maskwota kama hao kusalia mle msituni, ni njia mojawapo kati ya njia nyingi za kuchangia uharibifu wa msitu.

## 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu umechunguza na kudhihirisha kuwa kuna matumizi ya mikakati mbalimbali ya kipragmatiki katika diskosi za uhifadhi wa misitu zipatikanazo katika gazeti la *Taifa Leo*. Kuwepo kwa mikakati kama hii ya kipragamtiki katika diskosi za uhifadhi wa misitu huzua utata katika kufasiri makala husika ambapo maana iliyodhamiriwa na mwandishi wa diskosi hiyo hupotoka. Utafiti huu kwa hivyo unapendekeza kuwa waandishi wa makala kuhusu uhifadhi wa misitu wajitahidi kujieleza kwa kina huku wakifafanua baadhi ya mikakati ya kipragmatiki kama vile jazanda, kinaya, semi na kadhalika iliyotumika katika diskosi husika ili ujumbe uweze kueleweka.

Katika kulishughulikia swali lililouliza, ni njia zipi zinazotumiwa na umma kufasiri diskosi za uhifadhi wa misitu, utafiti huu uliweza kubaini kuwa kwa kweli kuna matumizi mbalimbali ya mikakati ya kipragmatiki inayotumiwa na umma katika kufasiri diskosi za uhifadhi wa misitu. Ilibainika kuwa baadhi ya fasiri kama hizo hupotosha maana iliyodhamiriwa na mwandishi wa makala husika. Utafiti huu unapendekeza kuwa wahariri wa gazeti la *Taifa Leo* wajitahidi kutoa tahariri zitakazotoa mwelekeo kuhusiana na makala juu ya uhifadhi wa misitu itakayokuwa imechapishwa katika gazeti hilo. Aidha, wataalamu wa uchanganuzi wa diskosi na ambao ni wasomaji wa gazeti la *Taifa Leo* watoe uchanganuzi wao kuhusu makala juu ya uhifadhi wa misitu katika gazeti la *Taifa*

*Leo*. Uchanganuzi kama huo ambao utafanywa na wataalamu hao utakuwa kama mwongozo wa kufuatwa na wasomaji wengine wa gazeti hilo.

Vilevile, uchanganuzi wa wataalamu wa uchanganuzi wa diskosi utasaidia katika kutatua tatizo la ufasiri wa kipragmatiki unaosababisha athari hasi katika shughuli za uhifadhi wa misitu kama ilivyobainishwa katika utafiti huu. Aidha, wanaisimu waliobobea katika lugha ya Kiswahili wanaombwa kujishughulisha na uandishi wa makala mbalimbali katika nyanja ya pragmatiki ili wasomaji waweze kuelewa na kuwa na uzoefu wa masuala yanayohusiana na nyanja hiyo na jinsi ya kufasiri diskosi kama hizo.

Katika kuchangia utatuzi wa tatizo la fasiri zisizosahihi za diskosi ya uhifadhi wa misitu, utafiti huu unapendekeza kuwa:

Tafiti zaidi zifanywe ambapo vitengo vingine vya isimu kama vile semantiki, mshikamano wa kileksia na hata isimu jamii vihusishwe katika tafiti hizo kama kihimili.

Idara ya misitu katika serikali ya Kenya iweze kushirikiana na wataalamu wa uchanganuzi wa diskosi ili waweze kusaidia katika shughuli za uhariri wa diskosi ambazo zinarejelea masuala kuhusu uhifadhi wa misitu na ambazo huchapishwa katika magazeti.

Inafaa kufanyike tafiti za diskosi za uhifadhi wa misitu ambazo aidha huchapishwa katika magazeti mengine mbali na gazeti la *Taifa Leo* au hutangazwa katika vyombo vya utangazaji kama vile runinga, mwingoya na kadhalika.

## MAREJELEO:

Allison, L. (2009). Conservation. Online: [http://www.answers.com/topic/conservation] (accessed 23rd October 2009).

Bloomer, A., Griffiths, P. & Merrison, J.A. (2005). *Introducing Language in Use, A Course Book.* Padslow, Cornwell: T. J. International Ltd.

Brenton, T. (1994). *The Greening of Machiavelli.* London: Eerthscan Publications Ltd.

Cotthem, V.W. (2009). New definitions of "forest" in global climate change agreements (IISD/N.SASAKI). Online: [http://dx.doi.org/10.1016/j.apenergy.04.04.015] (accessed 24th October 2009).

Dasgupta, P. (1993). *An Enquiry into wellbeing and Distribution.* New York: Oxford University Press.

Davis, S. (1991). *Pragmatics, A reader.* New York, Oxford: Oxford University Press.

Eggins, S. (2004). *An Introduction to Systemic Functional Linguistics 2nd Edition.* London: Continum.

Fairclough, N. (2004). *Discourse Analysis.* London. Routledge.

Garnhma, A. (1985). *Psycholinguistics Central Topics.* Routledge, London: OUP.

Gazdar, G. & Good, D. (1982). `On a Notion of Relevance`, in N. Smith (ed.) *Mutual Knowledge.* New York: Academic Press.

Gichiri, J. (2009, August 26). *Business Daily Kenya*: State could force farmers to plant trees on their land. Online: [http://allafrica.com/stories/200908260028.html] (accessed 24th October 2009).

Grundy, P. (2000). *Doing Pragmatics*. New York: Oxford University Press.

Grice, H, P. (1975). 'Logic and Conversation', in P. Cole and J.L. Morgan (eds) *Syntax and Semantics 3: Speech Acts*, New York: Academic Press.

Habwe J. & Karanja P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Harrison, P. (1996). *The Greening of Africa*. Nairobi: Academic Science Publishers.

Hofmann, R.Th. (1993). *Realms of Meaning*. New York: Longman.

Hornby, A. S. (2005). *Oxford Advanced Learner's Dictionary 7th edition*. Oxford: Oxford University Press.

Indede, F. (2007). 'Lugha ya Kitamathali katika Mahubiri ya Dini ya Kikristu.' Unpublished Ph.D Thesis. Maseno University.

Indede, F. (2009). The Pragmatics of Kiswahili Literary Political Discourse. The Journal of Pan African Studies Vol. 2, No. 8, March 2009.

Johnson, R. B. & Onwuebuzie, A. J. (2004). Mixed Methods Research: A Research Paradigm Who's time has come. *Educational Research*. Vol. 33, No. 7. Pp14-26.

Kasper, G. (1977). Can Pragmatic Competence be Taught. Online: [http://www.III.hawaii .edu/sltcc/Fa/Newsletter/Pubs.html] (accesed 3rd May 2010).

Kiss, A. (1990). *Living with Wildlife. Wildlife Resource Management with Local Participation In Africa*. USA. World Bank.

Larson, R. & Seagal, G. (1998). *Knowledge of Meaning*. Cambridge: Mit Press.

Lawal, R. A. et al, (1997). " A Pragmatic Study of Selected Pairs of Yoruba Proverbs." Journal of Pragmatics 27,pp 635-652.

Leech, G. (1983). *Principles of Pragmatics*. New York: Longman Group Limited.

Luvaha, J. (2009). 'Mshikamano wa Kileksia katika Insha za Kiswahili za Wanafunzi walio na Matatizo ya Kusikia katika Shule za Sekondari za Viziwi zilizoteuliwa nchini Kenya'. Unpublished MA Thesis. Maseno University.

Lyons, J. (1977). *Semantics*. Cambridge: Cambridge University Press.

Malinowski, J. (2012). The Pragmatic Interpretation of Utterances. Online: [http:www.home. umk.pl/../pragutter.pdf] (accesed 20th June 2012).

McLeod, S. A. (2008). Simply Psychology. Online: [http://www.simplypsychology.org/ qualitative-quantitative.html] (accesed 6th March 2012).

Mills, S. (1997). Discourse. Online: [http://www.answers.com/topic/discourse] (accesed 24th December 2010).

Mugenda, O. M & Mugenda, G.A. (1999). *Research Methods: Quantitative & Qualitative Approaches*. Nairobi: Acts Press.

Mulwale, B. (2005). 'Uhifadhi wa Mazingira Wilayani Bungoma.' Unpublished MA Thesis. Maseno University.

Nordquist, R. (2012). What is a Metaphor. Online: [http://www grammer.about.com-metaphor-definition and examples of metaphors-figures of speech] (accesed 22nd February 2012).

Ochwal, A. A. (2008). 'Communication Strategies Used by Non-Specialised Teachers of Deaf Learners in Nyanza Province.' Unpublished MA Thesis. Maseno University.

Okombo, O. & Habwe, H. J. (2007). *Pragmatic Strategies in the Use of Kiswahili Demonstratives*. Swahili Forum 14.

Omare, S.G. (2006). 'The Role of African Religion on Environmental Conservation in Kakamega District.' Unpublished MA Thesis. Maseno University.

Otiende, J. E., Ezaza, W.P. & Boisvert, R. (1991). *An Introduction to Environmental Education.* Nairobi: Nairobi University Press.

Rahayu, V. N. (2009). 'A Socio- Pragmatics Analysis of Promising Utterances in Barrack Obama's Campain Speeches.' Unpublished Research Paper. Muhammadiyah University of Surkarta.

Searle, J. (1962). *Speech Acts*. London: Cambridge University Press.

Shaozhong, L. (2004). What is Pragmatics. Online: [http://www.gxnu.edu.cn/../definition. html] (accesed 30th April 2010).

Sperber, D. & Wilson, D. (1995). *Relevance: Communication and Cognition*. 2nd edn. Oxford: Blackwell.

Strauss, A. & Corbin, J. (1990). *Basic of Qualitative Research*;Grounded Theory Procedures and Techniques. Newbury Park: Sage Publications.

Toili, W. W. (2000). 'Impact of Environmental Education on Secondary School Students: Perspectives of Environmental Quality in Bungoma District Kenya.' Unpublished Ph.D Thesis, Maseno University.

Touliatos, J. S. & Compton, N. H. (1988). *Research Methods in Human Ecology/Home Economics*. Iowa: State University Press/AMES.

Trochim, M. K. W. (2006). Purposive Sampling. Online: [ http://www.socialresearch methods.net/kb/sampnon-php] (accesed 30th September 2010).

UNEP, (1999). *Global Environmental Outlook 2000*. London: Earthscan Publications Ltd.

Van Dijk, A. T. (1981). *Studies in the Pragmatics of Discourse*. The Hague, Paris, New York: Monton Publishers.

Verschueren, J., Ola Ostman J. & Blommaert J. (1995). *Handbook of Pragmatics Manual*. Amsterdam, Philadelphia: John Benjamin's Publishing Company.

Wamitila, K. W. (2008). *Kazi za Fasihi. Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Muwa Publishers Ltd.